CKRC

VERBATIM REPORT OF

# CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KALOLENI CONSTITUTENCY, HELD AT MARIAKANI SECONDARY SCHOOL

ON

Monday, April 29, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KALOLENI CONSTITUENCY, HELD AT MARIAKANI SECONDARY SCHOOL ON 29TH APRIL 2002**

**Present:**

1. Com. Pheobe Asiyo
2. Com. Issac Lenaola
3. Com. Lethome

**Secretariat Staff in Attendance**:

Joash Aminga - Programme Officer
Rachael Kitonyo - Asst. Programme Officer

Patricia Mwangi - Verbatim Reporter
Eunice Kasisi - Sign Language Interpreter

**Meeting was called to order at 10.30 a.m. with Com. Pheobe Asiyo in the Chair.**

**Com. Asiyo:** Tuaanze mkutano huu wa leo na kabla, tujitambue kwa wale ambao wamefika kutoa maoni yao juu ya Katiba mpya. Tungependa kuuliza Muislamu mmoja, na Mkristo mmoja watuombee halafu tutaanza mkutano.

**Islamic Prayer: "**Eh Mola muumba wa bingu saba na ardhi saba tunakuomba kwa uwezo wako utupatie baraka katika mkutano wetu huu, tufaulu kama vile ambavyo wewe unaelewa mambo yanavyo faulu kwa baraka zako kwani wewe ndiye mwenye uwezo wa kila aina wkuweza kutufanikishia katika nchi yetu hii, pamoja na kiongozi wetu Rais Moi na viongozi wote ambao wako nchini yake wanaoipeleka serikali hii. Tunakuomba utujalie mipango yetu hii ya Katiba iwe ni mipango ambayo itafaulu, itakayowardhisha wengi katika raia mbali na kuwa hiwezekani kuwardhisha wote.

Tunakuomba utujalie kututilia baraka na wale mahasidi ambao wamesimama mbele yetu uwapatie balaha ambolo hazitafaulu zile hasida zao. Pia tunakuomba Mwenyezi Mungu utujalie katika maendeleo yetu ya nchi yetu hii yatunufaishi zote ambao tuko ndani ya nchi hii. Tunakuomba muumba bingu saba na ardhi saba, utufanie mafanikio yetu yawe ni mafanikio ambayo yatatuwezesha sisi tupate mafanikio ya nchi yetu hii sisi wenyewe vizazi vyetu vinavyo kuja na pia wale ambao wako mbele ya uwongozi wako Mwenyezi Mungu **(Arabic)** asante".

**Com. Lethome:** Tutapata maombi kwa ……………

**Christian Prayer:** Tuombe tafadhali, tuombe zote; "Mwenyezi Mungu uliyeumba bingu na nchi na vyote vilivyomo, tunakushukuru kwamba wewe ni kiongozi tunakusuru ya kwamba yoto yanatendeka kwa uongozi na madaraka yanayotoka kwako. Mungu wetu tunasema asante sana: wakati huu twajiweka mikononi mwako katika kufungua mkutano huu ili uwe pamoja nazi, amani yako ikawe pomoja nazi, utenge hila ya shetani iwe bali nazi, kwako peke yake tupate utulifu na amani. Bariki kikao hiki Mungu wetu ili yote wanaoyatayarisha kwa ajili ya Katiba ya kuiangalia nchi ipate mwongozo unaotoka kwako, ipate baraka kutoka kwako. Ukabariki viongozi walio hapa. Twamweka mikononi mwako Rais wetu kwamba awe akituzwa na kuongozwa na wewe mwenyewe, uweze kumpa umoja pamoja na wote wanaoshirikiana naye Kuitawala nchi yetu ya Kenya.

Mungu wetu wa utukufu ni wewe uliyeumba na siku zote unatulinda na kututunza na kutuongoza. Tunaamini Mwenyezi Mungu ya kwamba ukiwa pomoja nazi hapa, tutapata amani na uongozi wako utaweza kutuzaidia. Tuzaidie kufahamu sawasawa jinsi itakavyo kuwa sawa na raia wote wa nchi ya Kenya tukiamini ya kwamba yote yakitoka kwako binguni, yanakuwa mema kwa maisha ya wanadamu. Na kwa haya tunayo kuomba tunamini umeyasikia kwakuwa uko pamoja nazi hapa, utayatimiza sababu tumeomba katika jina la mwanao Yesu Kristo Mkombozi wetu; Amen.

**Com. Asiyo:** Asante sana mzee kwa maombi hayo hivi sasa tuko tayari kuwanza kusikiliza maoni ya watu wa Mariakani leo asubuhi, lakini kabla hatujafanya hivyo, ningependa kuwajulishini kwa wale ma-Commissioner ambao wamefika hapa kuzikiza maoni yenu, pamoja na wale wafanyi kazi ambao tumekuja nawao kuwandika kila kitu ambacho mtasema. Hapo kando pale mwisho huyo mama ni mtu wa kuwandika mambo yote vile mtakavvyosema kikamili kabisa, na pia atakuwa aki-record sauti zenu ili kwamba kile kitakacho toka kwa mindomo yenu au vinywa vyenu vizikisiwe vizuri sana mtu asije akafanya makosa. Na hapo katikati tuko na yule program officer wetu ambaye pia yuko na sisi hapa, na pale mwisho kuna yule msichana ambaye anatafusiri kwa wale viziwi na, wale wasio sikia ili pia wafahamu kwa lugha yao kwa vile kuna watu wengine ambao hawawezi kuzikiliza sisi kwa hiki kikao ja maana kabisa. Na hapa mwisho kuna msichana ambaye pia atakuwa akiandika kila kitu kile mtakacho kuwa mkiongea ili kusiwe na makosa yeyote.

Hapa mimi ni Commissioner Phoebe Asiyo na upande wangu wa kulia ni Commissioner Isaac Lenaola hapa mwisho ni Commissioner Ibrahim Lethome Asman ambao wote wako nazi hapa kuzilikiza maoni ya wale ambao wataongea leo. Tumepata majina ya watu saba kwa hivi sasa na tutaanza na Bwana Mohamed Mfaki halfu Ruth Mwakeo halfu Kutakuwa na Ali Mbaya, Bwana Isam Ali, Bwana Rajabu Simba, Bwana Eli Kondo na Bwana Patrick Kondo. Naona kuna muvua sijui Bwana coordinator, tungeingia ndani ya classroom, ili tusinyeshewe sana.

**Mohamed Mfaki:** Salaamu aleikum (arab) Mimi hapa nimesimama jina langu naitwa Mohamed Mfaki Mohamed mimi ni Imamu na ni Mwalimu katika Madrass Mazidinuru. Tasilimu Mazeras. Kitu ambacho nitakizugumzia zaidi ni kuhusu uongozi, utakaokuwa kuwa katika upande wa serikali yetu: Katika upande wa Katiba nigelipendelea na kuiomba serikali ikiwa kuna uwezekano, kwanza itambue itabu ambacho ni cha waisilamu ikiwa ni Kurani na kitabu hiki pia wakifahamu kwamba ni kitabu ambacho ndicho chenye mwongozo wa Kisilamu. Kwa hivyo waisilamu moja kwa moja Katiba yao wao ni Kurani. Hata katika historia tumepokea kwamba Yesu Mkristo ambaye ni Issa-bin-Mariam akija tena kutoka binguni, huyu atakuja fuata Katiba hii hii ya Kurani ambacho ndicho kitabu leo Waisilamu wanacho tumia. Kwa hiyo mimi ningeliomba serikali wale Waisilamu wawe wanatambulika katika kitabu chao hicho. Hicho ni cha Kwanza.

Kitu cha pili, tungeliomba wale wanaongoza katika serikali wawe ni watu ambao watafuata uadilifu kwa mfano leo katika mkoa wetu huu wa Pwani tunalia ngoa sana. Kuna kitu kama vile mfano Chuo Kikuu ambacho ninaimani katika Kenya hii, baada ya Nairobi, Mombasa ndiyo inafuatia lakini tumetamani mpaka leo na tunhamu ya kukipata chuo Kikuu. Kwa hivyo mimi kiupende waku ningeliomba tujengewe chuo hicho ambacho kitatuzaidia sisi na kutupunguzia taabu. Na kiupande mwingine tungeliomba serikali ifanye uadilifu.

**Interjection**: Interuption as a result of rain/leakages in the hall.

Nikiendelea na mpango kuhusu habari ya Katiba hii nileonelea kwamba hapa Coast panafaa kabisa tuwe na Chuo Kikuu. Kwa hiyo ningeliomba wahusika wajaribu kutupatia nafasi hiyo ili tupunguze kidogo matatizo yanayopata watoto wetu. Hii ilikuwa nimechangia katika upande wa Coast. Na pia nikizungumzia sana hii Katiba tungaliomba iwe kuna uzawa kati ya Mikoa ya nchi

hii ya Kenya. Isiwe kuna Mikoa inaboreshwa kuliko mingine yaani isiwe inakuwa bora kuliko mingine ili wananchi wasilie sana, kwani kulia kwa wananchi kuna sababisha kuizorotesha serikali.

Na kifungu changu cha mwisho kusungumzia ningeliomba kiongozi atakayechaguliwa katika Katiba yetu hii, yaani Rais iwe ni miaka mitano itoshe, na achaguliwe Rais mwingine kama kawaida. Na huyu Rais asiwe na ubaguzi awe ni Rais atakaye wapenda wote pasipo na ukabila ambabo tunajua ukabila ndio mama wa kufuja maendeleo na nadhani kwa hapa mimi nimetoselesha kwa mchangio huu ambao nimetua na ningeliomba wandishi kama nimekosea ni kawaida ya mwana-damu nami ni mmoja katika wana-damu salamu-maliakumu (Arabic).

**Com. Asiyo:** Upite hapa nyuma ili kuweka sahihi kwa hii register yetu kuonyesha kwamba umeongea hapa kikao hiki cha kutoa maoni. Sasa mama Ruth Mwako

**Ruth Mwako:** Hamjambo? Mimi ni Ruth Mwako ni mwalimu hapa na mtanisamehe nitaongea kwa lugha ya Kiingereza. Yangu mengi ni juu ya elimu, uchaguzi, na wabunge na kadhalika. Nitaanza kusema kuwa. "Those wishing to contest for the presidential seat from various parties should seek the consent of the wananchi six months before the elections time. Like now that we are having elections at the end of year, those who actually want to become President should have sort, or should seek for our mandate. That is what they should do six months before the General elections.

And those who are seeking for any Parliamentary or Civic seats should not have been charged in a court of law for any criminal offence we have heard case whereby people are charged and later acquitted and then they seek for Parliamentary or Civic seats so that they can protect the properties they stole from us. That is what we do not want. Kenyans should have a daily or weeklu roll-call of Members of Parliament that they have sent to represent them. We've had cases whereby out of the two hundred twenty twoMPs, there is always lack of quorum so Kenyans wonder what is happening with these two hundren and twenty two Mps,, where are they? Now in that connection, Kenyans should have a right to vote out their MP if they are not confident in their representation.

The Kenyan Cabinet should at least have five women Ministers at least holding key posts. We have always been heading social services every other time and it is like the men think that the women are only fit for social services; they think we cannot deliver in the key positions, and yet it is the woman actually who sends the men to Parliament or votes them as President or whatever: So at least there should be more Cabinet posts for the women. An MP once elected in any party into Parliament by the wananchi and he decides to defect to another party, because he has been influence or, has been induced with Kitu kikubwa-sio kitu kidogo, should not be allowed to contest in the by-electio, because it looks like he is not confident in himself. If he is voted in may be by KANU and then he decides, "Okay I want to represent the same people in DP". We don't want that person to go back, we are tired of these defections and reflections of such people.

And finally a Cabinet Minister should come from any party. It doesn't necessarily mean that a party that is ruling should be forming the Cabinet and the Cabinet Minister should also be a professional in that field. We have had areas whereby somebody does not fit to be may be a Minister of Education and we still have him there or may be doesn't even fit to be a Minister for Health and we still have him there. We don't want this thing. Can we have the people who are professionals actually becoming the Ministers in those portfolios. Thank you

**Com. Asiyo:** Thank you very much, sijui kama kuna maswahili?

**Com. Lenaola:** You are saying that candidates should seek the consent of the wananchi six months before elections; what is the mechanism for seeking consent, do they come to every District and talk to Kenyans or you want Kenyans to give a vote of what do you think at least every District must have a list of supporters, how do you want us to………..

**Ruth Mwako:** ………………Surveying those MPs so that they can be vetted, there should be a policy

**Com. Asiyo:** You are suggesting the Presidential candidates should actually be selected six months before the General election? Okay; The other thing I wanted to know from you Mama Ruth is this; you have said that Parliamentary candidates should be vetted for all that you said, how about Civic?

**Ruth Mwako:** The same for civic.

**Com. Asiyo:** Okay very good; now you also said that there should be rule of recall for members of Parliament who don't perform, in what sense?

**Ruth Mwako:** We had cases whereby there are MPs who are never may be in Parliament or if they are in Parliament, it is in very few sessions. So the wananchi do not know whether this individual actually is representing them in Parliament or he is doing his own business in Nairobi

**Com. Lenaola:** What is the percentage of voters you want to vote that they have no confidence - 10%, 90%?

**Ruth Mwako:** 90%.

**Com. Asiyo:** 90%.

**Com. Lethome:** Do you have in mind anything or an idea of how we shall avoid witch- hunting? Kwa sababu tunajua siasa za huku kwetu zilivyo, mimi nikishindwa Bunge, aliyeshinda akiingia kule, mimi nitanza hapo hapo kumwandama, kumuchipa ili

afanywe recall; sasa tutawezanje kuzuia mambo ya witch hunting?

**Ruth Mwako:** Okay, for a candidate who has lost election and then you hear this idea of witch hunting, I think the wananchi should also be able to realize the person who was defeated in a last General elections, should not be the person who is going round to induce them into saying that so and so is not performing.

**Com. Asiyo:** Sasa masaa ni mbaya sijui kama……nauliza Bwana Islam Ali, wa Mariakani, Muslim Society unataka kuongeza kwa niaba yao lakini kama una memorandum……………………………

**Islam Ali**: Niko na memorandum…………………….

**Com. Asiyo:** Haya basi kwa hivyo……………………..

**Islam Ali:** Na memorandum nataka niisome.

**Com. Asiyo:** A ah utaongea mambo yale ya muhimu kutoka kwa hii memorandum kwa vile sisi pia tutaisoma na pia tutaweka kwa Computer-word for word kwa hivyo hautapoteza; utakuwa umetuzaidia sana sana kwa maana umenena juu yake hakuna haja kuisoma nikutaja tu mambo muhimu maana hii yote itaingia kwa Computer.

**Islam Ali:** Salaam aleikum (arabic). Mimi ninawakilisha Mariakani Muslim Society kama Acting Secretary. Nimetengeneza memorandum ifuatayo; "Mariakani Muslim Society", na nitasoma kwa lugha ya kingereza. "Mariakani Muslim Society memorandum presented to the Constitution Review Commission on 29th April 2002".

Kadhi office; the appointment of Chief Kadhi and Kadhis to be approved by a body of Muslim scholars through interview. The said body of scholars should be constituted through Muslims' opinion, and that the office of the Chief Kadhi be expanded to include an Appeal Court; Any judgement on the said court of appeal must be final. That the holders of the said office should have all privileges of the (Arabic).

Citizenships; any child born by either of the two parents either father or mother who is Kenyan, should automatically qualify for Kenyan citizenship. A foreigner married to a Kenyan husband or wife should qualify for Kenyan citizenship. Kenyans must be allowed to have dual citizenship, that the citizenship should articulate that all Kenyans are equal, that they are all entitled to the rights and privileges regardless of their difference or belief, that question on the tribe and (inaudible) be avoided in all forms of application, that national document be issued under the said Act.

Land ownership; land ownership document be simplified and be accessible at the provincial level. The Constitution should

guarantee access to the said document to all landowners upon clarification. That any land issued with a title-deed upon a payment of a minimum premium should cease to attract any levies from councils or any other body. That all those acquiring land illegaly should forfeit the said land and be sued in the court of law.

Local authority; councils should be made autonomous and the elected Councillors should be empowered to run Council affairs. That any changes proposed to the council on charging levies or any other issue relating to it, must not be approved without consultation with the business community. In the event that the council fails to provide services on which it is obliged to, the business community should have a right to stop payment for any levies to the council, upon approval from the court. The minimum level of education for civic election candidates be 'O' level. The Chairman or Mayor be directly elected. To avoid corruption within the Council, all Local Authorities must publish their annual financial statements and make them available to the public.

National Assembly; Parliament should have powers to control its own calendar; that the dissolution of Parliament and the date for the General election must be de-linked from the Executive and be handled by Parliament. That any person with a criminal record must not be allowed to contest for a Parliamentary seat. That defection of members from one party to another must be checked, so as to save constituents the burden of going for by-election, or put them at the mercy of the MP.
Public positions; the appointment of senior members to Judiciary, the AG, Heads of Parastatals, and any other positions related to the above, must be approved by the Parliament. That holders of the said offices including Ministers, MPs, PCs, and any other related to the above must resign their positions in the event of them being incrimindated in any corruption charges. The retirees from government offices or any other related to it, must not be re-appointed to any other office.

Executive; the President should not be above the law and should be impeached in the event of criminal charges. The economy; the government must enhance all the economic resources in all areas. Income derived from economic resources of a particular region should have a high percentage of it remain in the same region, to cater for its development projects.

Freedom of worship; that freedom of worship must be guaranteed, that all institutions must adhere to this. That nobody should be compelled to go against his faith, that criminal charges be brought against anyone or institution going against this. Should the teaching of religious education be made compulsory in education at institutions, then the government must ensure that required teachers for the said subjects are deployed in all institutions.

Protection; that the government must at all times protect its citizens and any forms of discrimination be made a criminal offense. That any form of harassment of the public by the police, or any other organ of the State should be made a criminal offence. Thank you.

**Com. Asiyo:** Asante sana Bwana Ali; mimi niko na swali moja tu. Umezungumuza juu ya mambo ya uhuru wa kuomba, lakini

haujatueleza kabisa kwa vile siku hizi kuna watu wanao omba vyungu mbalimbali - kuna wale Satanic kuna wale wengine cult, je, ungesema hii freedom of worship iwe ni nani anapewa hayo maombi? Kama tutafanya worship tutamuomba nani?

**Islam Ali:** Nilisema Waisilam maombi ni kwa Mwenyezi Mungu peke yake and then Mumbajii wa sisi wote binadamu duniani.

**Com. Lenaola:** Iko swali kidogo tu kuhusu Chief Kadhi; umesema kuwa Makadhi wote wawe wanaangaliwa kama vile Judicial officers wengine. Lakini tukiangalia hawa Makadhi au Chief Kadhi pamoja na kuwa ni judicial officer, ana kazi zingine kama kiongozi wa Waislamu kama 'Mufti' wa Waislam. Wakati hamuwezi kuwandama yeye anatoa nchi zingine kuna Chief Kadhi na kuna Mfu sasa waislam wa Kenya mngependekeza tuendelee hivyo hivyo, Kadhi awe yuko kortini na mambo mengine. Yasiyo ya korti ay tuwe na ofisi nyingine ya Mufti?

**Islam Ali:** Mimi ningependekeza kuhusu mambo ya Waislam kwa upande wa kortini na kuhusu kuendeleza Uislam kwa jumla katika nchi.

**Com.Lenaola:** Ndio awekwe kama spokes person wa Waislam.

**Com Asiyo:** Si atakuwa na kazi nyingi sana?

**Islam Ali:** Ni pahali mpaka kwa sababu atakuwa amesoma sawasawa.

**Com.Lenaola:** Qualification ya kadhi ungetaka iwe gani?

**Islam Ali:** Qualification itategemea Muslim scholars ambao watakuwa wanamchagua; hao ndio wataamua.

**Com. Asiyo:** Asante sana Bwana Ali - Bwana Ali Mbaya amefika? Kama bado hajafika tutaendelea mbele. Kwa sasa tunamwita Rajab Simba ambaye anaongea kwa nafsi yake mwenyewe.

**Rajab Simba:** Ndugu, Makamishena habari zenu? Mimi ninazungumza kwa binafsi yangu.

**Com. Lenaola:** Endelea………………..

**Com. Asiyo:** Endelea twakungojea.

**Rajab Simba:** Mimi ningeomba Katiba itushirikishe sisi watu wa Pwani kwa mfano kama katika Ministry - na kama ni Permanent Secretaries katika Pwani, watu wetu wamepungua sana. Kuhusiana na serikali tumesema watu wetu wa Pwani

wamepunguzwa sana - wamenyimwa nafasi.

Pili, ningetaka katika kila Province, Company ikifunguliwa pale kuwe 65% ni watoto wa hiyo area ndio wanawekwa hapo. Sio kuwa Kampuni imefunguliwa hapa, vijana wa kwetu hawapati kazi hapa, vijana wa kwetu wanateseka hapa hapa lakini watu wanatolewa juu wanakuja pale kuendeleza kazi pale na watoto wetu wamesoma. Wengine hata wameenda polytechnic, ma-college mengine lakini pale hawapati nafasi hiyo. Hilo ndilo wazo langu la pili.

Wanzo la tatu, ningeomba kikosi cha Polisi kivunjwe kwa sababu kikozi cha polisi kwa kweli kinatenganisha serikali na wananchi, haza mkoa huu wa Pwani. Kilio changu kwanza ni Mariakani, Kaloleni, Changamwe. Kikoso hiki kimechukuwa watu wa Pwani kama si watu. Imekuwa kwamba wana uwezo zaidi wa kuingia nyumba za watu na kupekesheni without permission ambacho hicho ni kilio tulio nacho Mariakani kwanza halisi juu ya polisi. Kwa hivyo ningeomba kituo cha polisi kivunjwe kiundwe kikozi ambacho kitakuwa na amani kushikisha wananchi na serikali. Kile kikozi ambacho kitakuwa na amani. Hayo ndiyo maoni yangu sina zaidi, naona ni haya matatu tu.

**Com. Asiyo:** Asante sana Bwana Rajab Simba lakini pengine sijui ulikuwa unafahamu kwamba polisi ahawaruhusiwi kuingia manyumba ya watu bila kuonyesha identity yao.

**Rajab Simba:** Lakini wa Mariakani wamekuwa wako huru sana.

**Com. Asiyo:** Lakini ni heri ufanye repoti kwa mambo kama hayo kwa yule Mkuu wa hapa ndio afahamu kwamba polisi wanatesa watu

**Rajab Simba:** Hapa hakuna kitu, hapa kwetu Mariakani tumekuwa tumechukuliwa kama ni watu ambao hatuna maana, polisi anaweza kuingia any time kwa nyumba yako kwa sababu ya mnazi, anakuja nyumbani kwako anaingia through akiona mtu amepita hapo na mbono anakimbia nyumbani kwako through. Kwa hivyo sasa tumekuwa hatuna imani na serikali - sehemu hii yetu tumekaa sisi hatuna imani na serikali kwa sababu kwetu polisi hata waone mtu amekufu pale, hawatamfuata. Wakikuta gari ya mnazi imepita hivi, hao wanang'ang'ania kwenye mnazi. Mpaka imekuwa area ya Mariakanui hatuna imani na serikali kwa sababu wanasema serikali ndio mbaya na polisi ndio wabaya.

**Com. Lethome:** Basi ngoja nikuulize swali moja. Leo kwa mfano ungependa pengine kuwe mahali pengine unaweza kwenda kulalamika kuhusu polisi ama vipi. Kwa sababu kwa mfano kama leo hii ikiwa polisi amekudhulumu utakwenda wapi leo hii?

**Rajab Simba:** (Inaudible)

**Com. Lethome:** Sasa ungependa katika Katiba - chini ya Katiba mpya tuwe na mahali ambapo unaweza kwenda kulalamika

ikiwa polisi

**Com. Asiyo:** Bali sio kituo cha polisi………………..

**Com: Lethome:** Eh ambapo sio polisi - sio kituo cha polisi

**Rajab Simba:** ………human rights ikiwa kama hapa na ule haki wa binadamu tungeomba kituo kiweko kila mahali. Kwa sababu mateso yamezidi katika watu wa Pwani sana.

**Com. Asiyo:** Okay tumeshukuru sana unaweza kwenda pale ukajiandikishe kwa register yetu. Sasa tuko na Bwana Eli Kondo.

**Eli Kondo:** Mimi naitwa Eli Kondo na maoni nitakayotoa ni yale nimeyafikiria mwenyewe ni kama "Kondo's thoughts". Nikifikiria habari ya Katiba, kwanza nataka tuelewane kwamba Katiba ni ya watu wote na lazima iwe na usawa. Kwa hivyo nitazugumuza juu ya equality, ule usawa na division of resourses, powers of the ruler, na President mwenyewe na kitu kinaitwa Majimbo.

Kwanza tuaanze na huu usawa. Mimi ninafikiria kwamba tuliokosea pale mwanzo kwa sababu pale mwanzo tulipoanza kupigania uhuru ilikuwa ni tuwe sawa. Na kuwa sawa sote tulikuwa na shida moja – shida ya ugonjwa, ujinga na umaskini. Lakini vile maneno yalivyo kwenda, yalikuja yakaharibika katikati hapo - sijui ni wapi, lakini hivi sasa hayo mambo ni kama yameondolewa na tuko palepale.

Tuaanze na elimu; tukiangalia ni kwamba elimu ilikuwa kila mtoto Mkenya atakuwa na elimu. Sasa ilibadilika kwamba wengine wakaamka wakaendelea na elimu, sasa tunapata Professors na wengine wana Masters huko na mwingine hata hajaenda shule katika miaka 37 ya uhuru wetu. Mimi nafikiri hapo kulikuwa na makosa somewhere. Ningependa hivi; kila mtoto hapa Kenya, kama tunataka kuwa sawa, lazima aende shule ajue kusoma na kuwandika at least mpaka standard five; kila mtoto afike hapo standard five na isiwe kwamba tunawachia wafanye vile wanavyopenda kwa sababu tunajua wanavyopenda.

Kuna wazee wengine wana pesa za kupeleka watoto shuleni na hawataki, na hakuna mtu anaweza kuwafanya chechote. Sasa inakuwa imbalance. Yule mtoto wa fulani anaendelea - huyu mwingine mpaka 37 ya uhuru, mtoto mwingine hajajua. Anajua pale alipozaliwa. Na watu wengine kichumba kile kile kutoka uhuru mpaka sasa yuko palepale, hana njia kwa sababu hana mali. Tunasema elimu ni ufunguo, na mtoto ukimnyima ufunguo unataka aende wapi? Dunia hii ni pana sana. Ningetaka elimu iwe ya lazima at least mtu aweze ku-reason; eh kama wewe umepata Master's Degree na unaenda kufanya argument au discussion na mtu ambaye hajasoma kabisa ……………

**Com. Lenaola:** Ndugu yangu Eli wajua una dakika chache usingie kwenye mipango pendekeza.

**Eli Bondo:** Pendekezo ni kwamba watoto wote wasome na wakimaliza elimu kama standard five tunataka training - tunataka training okay. Wakishafika pale wafanyiwe mtihani. Wakishafanyiwa mtihani wale watoto, ile cream ichukuliwe isomeshwe na serikali. Wale ndio watu watakao endesha nchi na hawa wengine ambao wanabakia basi wanaweza kujitafutia risiki zao. Lakini wale ile cream ya Kenya iwe itapatikana kutoka kila mahali na si lazima kwamba twende shule na ma – uniform. Wanaweza kuwambiwa waje nchini ya mkoma serikali itoe mwalimu wale wengine waje wasome. Maanake tunataka waingize hapa maneno mengine.

Okay kitu kingine ni distribution of resources; mimi naonelea kwamba kila Mkenya ambaye yuaishi Kenya awe at least amegawigiwa angalau plot moja ya shelter. Because shelter ni kitu cha maana na huwezi kujiata Mkenya kama huna mahali hata ya kuishi.

Kitu kingine ni powers of the President. Nafikiria ni kubwa sana ile kuwa ni above the law isiwweko na kuwe na tume au board ambazo zitachagua watu sio President achague kila kitu -parastatals wote mpaka nchini; nafikiri hiyo ni powers kubwa sana kwa President. Kwa hivyo ikiwa tunataka tuendelee kwa njia sawasawa kwanza nafikiri elimu ndio kitu cha muhimu. Na sasa kitu cha mwisho ni juu ya Majimbo; Majimbo, tulianza serikali yetu na Majimbo na hatujui kwa nini ilikuwa discorded. Sasa watu wanasema serikali ni ya bara ya kwao – kuitia ubinafsi. Lakini tukiangalia zile seriklai zimeendelea na zile za majimbo, kwa mfano America, Canada, Germany – hizi zote hatuwezi kusema wao wako vibaya kuliko sisi. Lakini, seriklau yetu imetengana na Britain nayo haishindi hizi nchi tatu. Hii majimbo isituwe………………..kwa maana ndio (inaudible) maoja ambayo imafaa kwa serikali.

**Com. Asiyo:** Haya asante. Ningepende kuuliza swali moja. Je tukiwa na serikali ya Majimbo-yaani devolution of powers - umesema President ako na powers nyingi sana. Kwa hivyo unataka zipuuzwe. Lakini Majimbo unataka Majimbo kwa Province au kwa District au vipi?

**Eli Bondo:** Serikali ya Majimbo ni kwamba kila mtu atakuwa mahali pale yuko. Tuseme for example America, pale mahali mali yako iko nyingi zaidi, pale ndio mahali pako pa kuishi.

**Com. Lethome:** Sasa unataka hiyo iwe kwa mkoa au wilaya ndio jimbo?

**Eli Bondo:** Kwa Mkoa maanake ile ya kwanza tulitafuta hatukuipata kwa hivyo tukitaka tuipate tuikosoe………………………..

**Com. Asiyo:** Tunaelewa; asante sana. Ningependa uandikishe jina lako pale. Sasa tuko na Patricia Kondo; Asante mama karibu na utaongea na sisi kama upendavyo.

**Patricia Kondo:** Mimi ningependa sana kuzungumzia juu ya akina mama. Kina mama, ningependa Katiba yetu hii kwanza ianze kutuelimisha sote sawa - watoto wa kike na watoto wa kiume mpaka wawe darasa la nane tena bure. Sio iwe habari ya kulipizwa - tuwe tunafanya hiyo bure ili tuweze kuondoa huu ujinga ambao sana umeenea sana kwa akina mama, maanake hata akina mama kwa dakika hii wengi hawajui haki zao ni nini.

Ingine ni upande huu wa kwa mfano, kama huku kuna magogoni - wazee wale wanawekwa kuhukumu hizi kesi za magogoni. Ningependa hiyo ikiwezekana kuwe katika kila magogoni ikiwa kuna wanaume watano, wawili wawe wanaweke. Kwa sababu in most cases wanaweke wakienda kushtaki cases kwa magogoni, huwa hawatambuliwi sana na huwa hawaangaliwi vizuri kama vile ambapo waume wanapata. Ni nyingine Police, pia nigependa kama police pia wawe ni hivyo hivyo kama wako wawili katika station, waume ni watatu, na wanawake ni wawili. Maanake hawa wanawake wawe wana represent wanawake wakija pae kwa station.

Na nyingine ni mambo ya urithi sasa; Urithi wanawake wananyanyaswa sana. Ningependa tuwekewe sheria ya kutufanya sisi kina mama tuwe tunaweza kurithi mali. Lingine, ninasema ni kama itawezekana Katiba iweke muda hii case ya kuwa "come we stay" - at least watu wakikaa kama miezi sita kama bwana na bibi, iwe sasa inaithinishwa kuwa sasa hao ni bwana na bibi, na hawawezi tena kuwachana maanake hii inadhurumu sana wakina mama. Lingine ni juu ya ma-mayor hawa Tungependa Katiba iwe kuwa Mayors wanachaguliwa na wananchi wenyewe. Sio ma- Councillors kuchagua ma-Mayors - lakini wananchi wenyewe wanaweza kuchagua ma-mayor wenyewe. Nafikiri hapa nimefika mwisho.

**Com. Asiyo:** Asante sana mama Patricia kama …………………..

**Com. Lenaola:** Swali ndogo kuhusu mambo ya "come we stay" umesema kama wakiishi pamoja baada ya miezi sita, automatically iwe bila sheria yeyeto bila kidhinishwa vyovyote vile kulingana pengine na dini……………….

**Patricia Kondo:** Sasa hapa ikimalizika miezi sita, walazimiswe wawe wataunganishwa pamoja, sio ije kuwa watakaa miezi sita halafu wakosane pale mama pengine ana mtoto itakuwa ni vibaya zaidi.

**Com. Asiyo:** Jiandikishe pale. Kama Bwana Ali Mbaya hajafika, basi tutaongeleshwa na Bwana Mohamed Ibrahim, Bwana Isaac Ali kuna Isaac Ali, kama bado yuko njiani ……. Shaban Ali.

**Shaban Ali:** Mimi ningependa kuchangia kuhusu Katiba, mambo matatu peke yake. Kwanza, kuna upande wa hii investments - serikali yaita watu waje wafanye investment hapa Kenya. Lakini wakija, ajabu ni kwamba katiba haiwalindi, au hailindi masilahi ya wananchi. Utakuta mtu ametoka huko Uganda amekuja kujenga kampuni hapa, anajenga anamaliza anaenda kuchukuwa wafanya-kazi wote kutoka Uganda anawaweka hapa. Wale wale watu wa pale, wanakuwa hawapati kazi. Kuna

kampuni karibu tatu hapa Mombasa ziko namna hiyo. Ukifika pale unaambiwa wewe si mtu, wewe nenda ukaajiliwe kazi Tanzania ama uandikwe kazi Uganda. Na ukingalia Kampuni imejengwa hapa hapa katika serikali ya Kenya ambako Katiba iko inalinda masilai na hakuna mtu anafaidika hapa. Kwa hivyo, hii katiba itakayoundwa sasa, ihakikishe mtu atakayekuja atengeneze Mapuni yake apewe masharati kuwa atachukuwa wafanya kazi - achukue 90% kutoka hapa hapa Kenya na hiyo percentage itakayobakia achukue kwake sio yeye jenge Kampuni hapa kisha akachukue wafanyi-kazi huko, sisi tutapata taabu.

Jambo la pili kuna mambo ya water billing - mambo ya kulipa maji. Utakuta katika hii Coast Province ukipiga hesabu hapa katika Province, watu wanalipa maji in cubic meters, ambapo hii cubic meters hiyo ni pesa nyingi ukilinganisha na Provinces nyingine wanavyolipa. Kwa hivyo Serikali hiyo itakayoundwa ama hii Katiba itakayoundwa ihakikishe kuwa kila Mkoa unalipa maji kisawasawa - kama huku ni millimeters huko ni millimeters kama huku ni cubic meters huko ni cubic meters, sio huku walipe hivi huko walipe hivi - hiyo itakuwa hakuna usawa na itakuwa ni fujo tu kila wakati, hawa wanalalamika hawa wanalalamika.

Jambo la tatu ni kuhusu program limitation katika KBC. Tunajua kweli kuna dini tofauti tofauti na kila dini inajipigania kivyake. Lakini sasa at least, hii Katiba iwe na mpangilio fulani, kuwa "nyinyi leteni wathamini wenu ikifika wathamini fulani wacheni". Sio huyu anakuja tu - kama kwa mfano sisi Waislam kuna kipindi kimoja tu katika KBC ambacho ni "Uliza ujibiwe" na kinafanywa only Fridays peke yake. Kwingine kote unasikia tu ni kipindi cha Christain - hatukatai lakini kuwe na program limitation; huku kuwe na vipindi vitatu huku vitatu, huku viwili huku viwili ili kila mtu apate ule usawa wa kitaifa.

Jambo la mwisho mimi ningependa kuchangia tu kuhusu upande wa nani – Viongozi. Viongozi watakaochaguliwa wawe tu wadilifu. Atakayekosa uadilifu awe disqualified hapo hapo. Kama ni kwenda kufungwa, kama ni kuwachishwa kazi, awachishwe lakini sisi tunataka uadilifu maanake kukosa uadilifu ndio kunaleta balaa katika Serikali. Kwa hivyo yangu mimi ni hayo tu.

**Com. Asiyo:** Asante sana Bwana Shaban Ali, ujiandikishe pale kwa register. Sijui kama Bwana Ali Mbaya amekuja; tutamngojea. ………… Point ambayo mko nayo kwa maisha yenu tangu utotoni. Na hatujawahi kuwandika katiba kama wanakenya. Huu ndio wakati tutaweza kuwandika katika yetu na usifikirie kwamba wewe maoni yako ni madogo – tafadhali kila mtu aliyefika hapa atueleze kile ambacho anataka kibadilishwe kwa Katiba hii mpya ili uwe na nafuu na uhuru ambao pengine hujaweza kuwa nao. Usirudi kutoka hapa bila kutoa maoni yako tafadhali.

**District Co-ordinator:** Mimi nataka kuwajulisha kama mwenyeji wa huku kwamba hili ni jambo ambalo - na kulingana na vile ratiba ya Tume kwamba walikuwa wanakuja kwa wananchi wenyewe, wasikie kutoka kwa wananchi wenyewe na wala sio wao kwenda kuketi tu na kuzungumza sheria na mambo kadha wa kadha. Kwa hivyo hii ni nafasi ambayo imekuja kwenu na mkiachilia, msije tena mkasema mbona walikuja na mambo yamekuwa hivi? Lile jambo lako ndogo ambalo unaliona ni ndogo

laweza kuwa kubwa katika kuchangia. Kwa hivyo ni wajibu wenu msije kuwa watu wa kusikiliza; tusikize na pia tutoe maoni ili hawa wametoka huko waweze kurudi kusema kwamba watu wa eneo la Mariakani na karibu karibu, haya ndio waliokuwa nayo. Lakini kila mtawaacha waondoke na mawili, matatu tutakuwa sasa hatuwambii chochote tunajiumiza sisi wenyewe kama wananchi. Kisha tunasema mbona hatukuhusishwa hili ni jambo letu; Com. Lethome ameshaeleza hakuna atakayeshtakiwa, hakuna atayefungwa - sema bila uoga.

**Com. Asiyo:** Asante sana. Kabla Bwana Eli hajaongea nataka tu kusema kuwa hivi leo sisi hatutaongea. Hatukuja hapa kuongea na nyinyi bali tumekuja kusikiliza maoni yenu pia vile mngependa Katiba mpya iiandikwe. Na kwa hapo, ningepende kuuliza Commissioner Lethome awaeleze zaidi.

**Com. Lethome:** Kama alivyosema Commissioner mwezangu ilikuwa leo si siku yetu ya kuzungumza. Tumemaliza Mkoa wa Kati ambapo tuliwasikiliza watu, na tumeingia katika hall mmoja mahali panaitwa Karatina Mathira, ndio sehemu ambako watu walizungumza kwa wingi sana. Lakini kwa sababu tunaona majina ya wale ambao wanaotaka kuzungumza ni machache sana, kidogo tumepigwa na mshutuko kidogo, na imekuwa hakuna bundi lazima tuwazungumzie.

Kwanza nataka kuwaambia hivi: Tangu tulipopata uhuru imepita miaka zaidi ya thelathini na nane. Ninataka kuuliza watu wa Mariakani na muniambie wazi wazi - hapa hakuna kujifichana. Nani baba yake ama wale ambao wamefikisha umri wa miaka arubaini aleyehuzisgwa katika Katiba hii ambayo inatutawala sasa? Maoni yenu yalikuja kuchukuliwa? Nani kati yenu alikuwa Lancaster hapa? Baba ya nani alikuwa Lancaster hapa? ……….Mzee Perus alikuwa Lancaster? Maoni yake yalichukuliwa katika hii Katiba? Kwa ufupi Katiba inaotutawala miaka thelathini na nane au zaidi, hakuna Mkenya ambaye aliombwa maoni yake katika hiyo Katiba. Sasa tumengoja miaka thelathini na nane au thelathini na tisa, tumepewa fursa ya kusema wananchi mnataka mtawaliwe vipi. Kila mahali ukienda utasikia wananchi wanalalamika. Juzi juzi tumetoka Mkoa wa Kaskazini Mashariki (North Eastern Province) wao hata hawaamini wako Kenya. Ukitoka huku ukienda huko wanakuuliza habari za Kenya, na kwa sababu ya nini? Lami Mkoa mzima ni kilometer sita peke yake, hawana maji, hawana nini. Hata polisi walioko huko ni tafauti na polisi walioko huku kwetu wanavaa uniform tofauti zile - za jungle. Hawavai namna hizi zinaitwa Service Numbers - hawavai kabisa, wao wanakuuliza habari za Kenya. Na kila mahali ukienda hakuna Mkenya ambaye halalamiki. Labda watu wa Mariakani ndio tu hamna malalamishi yeyote. Hamna malalamishi nyinyi?

**Audience:** Tunayo

**Com. Lethome:** Sasa nataka kuwaambia hivi; hii fursa tumeingoja miaka thelathini na nane na baada ya vita vikubwa. Zaidi ya miaka kumi, watu wananga'ngana sheria ikabuniwa ya kuwapa wananchi nafasi ya kubadilisha Katiba. Mimi ninajua Waisilam wanaamini kuwa kila kitu kufanywa na Mwenyezi Mungu, ama sivyo Waisilam? Na Wakristo pia mnaamini kila kitu kutoka kwa Mwenyezi Mungu ama sivyo?

**Audience:** Ni hivyo.

**Com. Lethome:** Tuchukueni mfano tu wa riski. Riski yako inatoka kwa nani? Inatoka kwa nani? Semeni msiogope.

**Audience:** Kwa mwenyezi Mungu.

**Com. Lethome**: Sasa ninataka kwanzia kesho ulale nyumbani kwako umuombe Mwenyezi Mungu akuletee sima kitandani, itakuja?

**Audience:** Haiji.

**Com. Lethome**: Kwa dini ya Ki-Islamu twasema hiyo ni haramu kwanza. Kulala kitandani ungojee riski yako ni haramu nafikiri kwa Waisilam na Wakristo. Sasa ikiwa wewe utakaa nhini halafu utarajie kuwa mabadiliko yatatokea, unajidangaya. Akiingia Simba saa hizi hapa, mtangoja ama mtakimbia? Semeni mtakimbia ama hamtakimbia?

**Audience:** Tutakimbia.

**Com. Lethome**: Kwa nini msimwachie Mwenyezi Mungu awalinde kutokana na huyu Simba? Sasa ndio nawaambia hivi, hii fursa ikipita ni kama kuwa umedhulumiwa miaka thelathini na minane na bado uko tayari kudhulumiwa.

Waisilamu nitawakumbusha. Tunaambiwa katika dini hakuna kudhulumu wala kukumbali kudhulumiwa (Arabic) hiyo ndio dini. Usimdhulumu mtu wala usikumbali kudhulumiwa. Tukikaa kimia sasa ni kama kuwa umeridhika na hukumu ya miaka thelathini na minane na unawaambia “endeleeni tu”. Au unasema “aliyedhulumiwa sio mimi ni mwingine kwa hivyo aliyedhulumiwa wacha azungumze”. Halafu mimi najua wasi wasi ya watu wengi wanasema mambo wa Katiba ni mambo ya sheria tuwachie wanasheria watengeneze Katiba. Mimi nawaambia hivi hapa Mariakani na Nairobi ni wapi kuna maofisi yenye starehe zaidi?

**Audience:** Nairobi.

**Com. Lethome**: Nairobi kuna air conditioner huku, ofisi nzuri nzuri, viti vizuri vizuri vya kuzunguka, twazunguka navyo hakuna balaa nyinyi. Kwa nini hatukukaa huko takaandika Katiba? Wiki moja tu tutakaa chini tutaandika Katiba wanasheria. Lakini tumesema tunataka Katiba ya wananchi watoe maoni yao. Sasa tunawambia si lazima uwe mwanasheria, hatuwezi kuwa na wanasheria milioni thelathini, - haiwezekani. Nchi ya wanasheria itaharibika, ikiwa ni wanasheria peke yao.

Wewe mama zungumuza kwa lugha ambayo unafahamu. Sisi tutachukuwa hiyo lugha yako tutaibadilisha ki-Katiba. Nitawapa mfano mnajua Waluyha; Waluyha kuna chakula wanakipenda sana - kuku. Unajua kuku? Tulipoenda Bukhungu Stadium

tulisema wacha tujaribu tu kuwauuliza hawa kama wanajua. Tukamwita mama mmoja kikongwe tukamuliza, "mama hebu sema; tumekuja Kurekebisha Katiba hebu sema taabu yako"? Akasema, "taabu yangu mimi nataka mzuie Chief kuchukuwa kuku wangu bila ruhusa yangu". Tena hata kuku alimuita kwa Ki-luyha "ingokho" hakumwita kwa Kiswahili. Watu wakashangaa huyu mama anambia Tume imetoka Nairobi, anakuja kuwambia habari ya kuku na Chief! Mama alitumia lugha yake kutuambia kuwa anataka Katiba ambayo itaniakikishia mali yangu yameifadhika, kuku ni mali ihifadhiwe. Na pia alizungumza point mbili – Nataka pia Chief mamlaka aliyopewa asiyatumie vibaya. Ni Katiba ama hiyo si Katiba?

**Audience:** Ni katiba

**Com. Lethome**: Watu wa Mariakani amkeni bwana; haya tukaenda Embu mama mmoja alikuwa ananyonyesha mtoto wake, tukamuuliza "Mama, shida yako ni nini wewe katika nchi hii?" Alisema kwa Kikuyu "ndirenda irio cia mwana" - "nataka chakula cha mtoto". Maanake kikakatiba ninataka Katiba itanihakikishikia basic needs, chakula ni katika mahitaji ya kimsingi ama sio katika mahitaji ya ki-msingi? Sasa watu wa Mariakani lugha kama hiyo imewashinda kweli kuzungumza? Sasa ndio nawambia kama mmeridhika na dhuluma ya miaka thelathini na minane, kwa nini mkubali vizazi vyenu vijavyo vidhulumiwe miaka mia mbili ijayo? Kwa sababu hii nafasi haitakuja kesho kutwa au baada ya miaka miwili. Pengine tutangoja miaka mia moja au miaka mia mbili. Kwa hivyo ndio nawambia hii nafasi msiwache na mseme waliozungumza wanatuwakilisha sisi – La! Saa hizi nikimwambia kijana yule simama, nimuulize shida yake, atasema "Nimemaliza shule miaka mitatu bado nina-tarmac sina kazi". Hiyo ni shida ama sio shida? Inaweza kushugulikiwa ki-katiba ama haiwezi?

**Audience:** Inaweza.

**Com. Lethome**: Sasa mnangoja nini? Ongeni; Asanteni

**Com. Asiyo:** Nafikiri mumepata mawaidha ya kutosha kutoka kwa Commissioner Lethome na ningependa kuimiza sana kwamba kila mtu aliyeko kwa chumba hiki asitoke hapa leo bila kuongea jambo lolote ambalo linamdhulumu yeye. Kama ni mambo ya afya, elimu, Serikali yenyewe, chakula, kuolowa, ndoa na talaka - kila mtu aliye hapa leo - au kukosa kazi, twataka mtueleze haya yote ambayo unaona katiba itaweza kuwasaidia.

**Interjection:** Inaudible.

**Com. Asiyo:** Bwana Kondo wewe ushaongea.

**Bwana Kondo:** Nishaongea, lakini kitu kidogo tafadhali ukiniongeza dakika tano…

**Com. Asiyo:** Na tutaona tukipata nafasi utarudi…………….

**Bwana Kondo:** ……..wakimaliza wenzangu……….

**Com. Asiyo:** Na wewe Mzee una jambo gani?

**Mzee:** Mimi nasikitika kwamba hatukufahamishwa Mariakani kama kuliwa na Ma-Commissioners watakuja kuwangalia Katiba. La sivyo, ningewaomba pia mtueleze ni utaratibu gani mmetumia kuleta hii habari kwetu. Kwa sababu majina yaliofika hapo na tulioko hapa ni tofauti.

**Com. Asiyo:** Asante; hebu nikueleze utaratibu ambao umetufanya tufike hapa ni kwamba tulipokuja hapa kuwaeleza juu ya Civic Education, tuliwambia kwamba baadaye Ma-commissioners kadhaa watafika hapa kuchukuwa maoni ya watu wa hapa Mariakani. Na ndio tumekuja kufanya leo na tumetangaza kwa radio, magazeti zote na pia hata jana, Councillor wa hapa pamoja na Coordinator wenu walizunguka kote Mariakani wakieleza watu kwamba leo hii tutakuwa na kikao.

**(Grumbling from the Audience)**

**Com. Asiyo:** Basi kama sivyo, kama hamukusikiliza radio na pia humukuweza kusoma magezeti ni bahati mbaya lakini tutaendelea na wale waliofika hapa na tungependa kila mmoja - naona kama watu hamsini hapa - kwa hivyo watu hamsini ni wengi kama mna maoni mtatoa kila mmoja, ili msitoke mkisema kwamba hamukupata nafasi ya kuongea.

**Com. Lenaola:** Kuna form hapa ambayo tutaizungusha, tukiuliza kama unataka kuzungumza hutaki. Na ukitaka kuzungumza, uko na barua, ama utazugumuza kwa mdomo ama utazugumuza kwa lugha gani, tuna kibarua. Kwa hivyo kama utazungumza sasa hivi hii barua jiandikishe tutakwita. Watu wale tumeitwa walijiandikisha mbele sana kabla sisi kufika. Mwenye anataka kuzungumza kuna barua hapa.

**Com. Asiyo:** Tafadhali kila mtu ajindikishe hapo na aongee ili tupate mawaidha kutoka kwenu vile tutaandika Katiba hiyo mpya. Kwa wale ambao wanaingia sasa tafadhali jiandikishe pale ili mje mukatuongelesha juu ya Katiba mpya ambayo mnaitaka nyinyi wenyewe - karani wenu yuko hapo hapo. Asante sasa tutamsikiliza Bwana Kimamo Mathew.

**Kimamo Mathew:** Asanteni; nitaongea kwa Kingereza. The first one is on the President. I am saying the President should have at least 50% of the cast votes and is the one to replace the one of the 25% in the five Provinces. Then he must also name the Vice President who shall be his running mater thus giving him security of tenure. Then, the Presidential, Civic and the Parliamentary elections should be done separately. Preferably the Civic and the Parliamentary done first and then the Presidential done later. Then at least, the President should have at least a degree.

Then on the employment: Employment and recruitment should be done on merit for example if the cut-off point for the

University is a C+ of 6.6, then the next category that is done by the Public Service Commission should be done from – for examle, if it is in the Ministry of Education, the diploma intake should be done from 6 .5 and also be given a cutting point rather than saying it is just C with a C- in a particular subject. I feel also that there should be no quota system for the national schools. Let it simply be the best. Then let the national schools be distributed in all the Provinces, not being concentrated in one area. Then, I have a feeling that also we should have schools for the talented students. If a student is found to be exemplary good in electronics let him be given a chance by being taken into a special school, which gives him all those facilities that he might require.

Then the office of the Attorney General, the Chief Justice and this other Government senior offices, should have a security of tenure, and subjected to a 75% votes of the Parliament. I think that is all I had.

**Com. Lenaola:** ……….it's not clear what he means by 25% during Provinces we retain it or we remove it.

**Kimamo Mathew:** We retain it and then we add 50% of the cast votes

**Com. Asiyo:** Votes for the Presidential candidate

**Kimamo Mathew:** For the Presidential candidate.

**Com. Asiyo:** And then you talked about very complicated education for the Presidential candidate like you want them to be people of University degrees?

**Kimamo Mathew:** At least a university degree

**Com. Asiyo:** At least a university degree; thank you Kimamo Mathew, sasa tuko na nafasi ya kusikiliza watu wengine ambao kwa sasa washaweka majina yao. Kina mama tafadhali msije mkatoka hapa bila kuongea halafu mtasema tunanyanyashwa sana huko nyumbani……… Tafadhali sasa, naona Bwana Ali Mbaya naona ameingia, anaweza kuongea sasa. Uliweka jina tangu asubuhi sijui umepotea wapi Bwana Ali Mbaya.

**Ali Mbaya:** (Inaudible conversation).

**Nazib Fakil:** Mimi nauliza powers za Rais**,** na za Bunge, na za Mahakama ziwe ni vitu tafauti kabisa vizishikane hata kidogo kwa sababu, shida zote ambazo tunapata ni kwa sababu Bunge ambayo tulichagua ituhudumie, ni Bunge lakini show-off. Yaani Bunge ambalo halina kazi ni kitu kimewekwa pale tu kwa maonyesho na hii ni kwa sababu hawana uwezo na wala hawatakuwa na uwezo. Kwa sababu Tume ambayo inasimamia uchaguzi ni Tume ambayo imechaguliwa na Rais. Bunge liko chini ya Rais.

**Com. Asiyo:** Wewe twambie vile ungependa – pendekezo lako tu.

**Nazib Fakil:** Na mahakama vile vile………………..

**Com. Asiyo:** Twambie vile unataka iwe.

**Nazib Fakil:** Kwa hivyo kila body ikifanya kazi peke yake, litakuwa ni jambo la kisawa sawa, na yale ambayo twayataka yatakuwa ni mambo ya kunufaisha. Kwa jumla, "watachambua watu mengi sana". Lakini kwa jumla, ni Katiba hii ambayo iliandikwa kutoka wakati wa mkoloni, ndiyo ambayo yataka ibadilishwe yote ili tupate Kenya mpya. Hii ndiyo summary- we have to change the whole Constitution to get a better Kenya. Thank you.

**Com. Asiyo:** Lakini twambie tutabadilisha namna gani? Wataka tuibadilishi aje?

**Nazib Fakil:** Tubadilishe…………………………….

**Com. Asiyo:** Umeongea juu ya mambo kama ya nguvu ya President…………………..

**Nazib Fakil:** Separation of power…………………

**Com. Asiyo:** Seperation of power?

**Nazib Fakil:** Yes.

**Com. Asiyo:** Haya hakuna mambo mengine unataka kusema juu ya………………

**Nazib Fakil:** Hiyo kama itaondelewa itakuwa ime play 50% of the whole thing

**Com. Asiyo:** Haya.

**Com. Leneola:** Sawa. Sasa swali hapa; umesema - Jamani hebu tusikizaneni hapa, tusikizanani uenda tukapata faida kwa yale yanayozungumzwa. Umesema tuwe na Tume ya uchaguzi ambayo ni huru. Sababu ilioko hivi sasa inachaguliwa na Rais. Pendekezo katika Kenya mpya, Tume ya uchaguzi ichaguliwe na nani?

**Nazib Fakil:** Tume ya uchaguzi ichaguliwe na viongozi katika Provincial level

**Com. Leneola:** Viongozi wa kisiasa?

**Nazib Fakil:** Organization za kidini – naam.

**Com. Asiyo:** Kuna kitu kingine tena ungetaka kusema na hujasema usije ukarudi nayo moyoni?

**Nazib Fakil:** No, am okay.

**Com. Leneola:** Nitamsukuma atasema lingine. Umesema kuwa mahakama haina uhuru hivi sasa?

**Nazib Fakil:** Haina uhuru.

**Com. Leneola:** Unajua Chief Justice hivi sasa anachaguliwa na President.

**Nazib Fakil:** Ndio.

**Com. Leneola:** Na ma-judge wa mahakama kuu. Katika Kenya mpya ungetaka tuendelee hivyo hivyo ama wawe wakichaguliwa na nani tena?

**Nazib Fakil:** Kuwe na mabadiliko wachaguliwe na any body ambayo itakuwa formed lakini iwe kutoka Bunge au kutoka - lakini iwe another body.

**Com. Leneola:** Basi ungependa wewe kama mMuislamu;

**Nazib Fakil:** Ndio;

**Com. Lenaola:** Wewe kama Muislamu ungependa Makadhi wawe na hitimu gani ama elimu gani? Kadhi wa Mombasa ama Chief Kadhi wawe na elimu gani ya Kiislam?

**Nazib Fakil:** Hapo kuna matatizo ya elimu - tuna Makadhi wengi ambao wamesoma Quran lakini kidunia hakuna………………..

**Com. Lenaola:** Ungependa ……………..

**Nazib Fakil:** Eh na hata huyu aliyoko anao elimu ya ki-dunia…………………………..

**Com. Leneola:** Wacha aliyeko Bwana…………….

**Nazib Fakil:** Lakini twataka Kadhi atayekuja awe ana elimu ya dunia na ya Quran.

**Com. Leneola:** Kiwango gani, standard one, standard two……………….

**Nazib Fakil:** University level;

**Com. Leneola:** University okay. Rais sasa ana mamlaka mengi ama?

**Nazib Fakil:** Ana powers nyingi sana kupita kiasi

**Com. Leneola:** Sasa ni kama zipi ungetaka ziondolewe

**Nazib Fakil:** Kama number sita ya kifungu cha Katiba ya Kenya ya zamani. Anasimamia fedha zote, na anachagua yule mwenye kusimamia fedha.

**Com. Leneola:** Wachaguliwe na nani?

**Nazib Fakil:** Sasa tungependa ibadilishwe kuwe na body nyingine ya kuchagua mambo kama hayo kuhusu kifedha na nini

**Com. Asiyo:** Kama body gani?
**Nazib Fakil:** Kama Parliament.

**Com. Asiyo:** Mambo ya kina mama hujaongea?

**Nazib Fakil:** Sikukaribishwa lakini ukinisukuma nitasema.

**Com. Leneola:** Bunge letu tungu tupate uhuru mpaka sasa tumepata Waziri wa kike mmoja tu - mwanamke mmoja; na sasa hakuna. Kuna usawa hapo tuendelee hivyo hivyo ama unaona kuwe na mabadiliko?

**Nazib Fakil:** Hapa mimi mingewalaumu wenyewe kina mama, kwa sababu kutoka Rais mpaka mtu wa chini kabisa anachaguliwa na mama.

**Com. Leneola:** Pendekezo sasa.

**Nazib Fakil:** Kwa hivyo ni wao wenyewe kina mama waungane walete mwamuko kiupande wao. Hapa wasilaumu mtu.

**Com. Leneola:** Kuna nchi kama Uganda, wanaifadhi viti fulani ni za kina mama – reserved seats za akina mama na kuna kitu kinaitwa "affirmative action" ambayo inasema tuwe kuna uakilishi wa akina mama, at least Bunge iwe 2/3 ya kina mama ungependeza iwe hivyo?

**Nazib Fakil:** Mimi reservation si support, sababu uki-reserve mtu kitu utamfanya ana kuwa reluctant – hashuguliki. Lakini asi-struggle yeye achukue, hiyo ni mzuri. Lakini reservation si support.

**Com. Leneola:** Kusiwe na reservation?

**Nazib Fakil:** Hakuna reserve. Halafu matatizo makubwa sana ambayo yatukumba hapa, ni kutokuelewa; Hii Tume imekuja hapa kutafuta mageuzi ya Katiba. Lakini kutokana na kukaliwa kwa siku nyingi unashindwa kuelewa pia, unaanza kueleza shida zako. Mwaweza kuona problems kama hizo

**Com. Leneola:** Sasa hizo shida hebu tupatie.

**Com. Asiyo:** Mnataka aje?

**Nazib Fakil:** Twataka sisi watu waelewe zile haki zao, na wajue wanaenda vipi.

**Com. Leneola:** Unataka wafundishwe katika makao gani - kuwaanzia skulini hapo au?

**Nazib Fakil:** Kuwaanzia skulini na vyombo vya habari pia.

**Com. Leneola:** That's all.

**Com. Asiyo:** Haya asante.

**Nazib Fakil:** Asante.

**Com. Asiyo:** Sasa tuko na Bwana Kalama John, C.C.C Secretary. Bwana Kalama John karibu.

**Kalama Alphonce John:** Kwa jina mimi ni Kalama Alphonce John, ni mwandishi wa Kaloleni Constituency Constitutional Committee. Nataka kuchangia macheche tu. Tukizungumza mfumo wa ki-serikali - structure of Government; Mimi naona mfumo ambao uko sasa hautufai. Unitary Government itufai kwa sasa na naweza kuseama kama haikupitwa na wakati, basi inaendelea kupitwa na wakati. Ningeomba ikiwezakana, tubadilishe tuwe na Federal system of Government. Tugawanye mamlaka kuwe na Serikali kuu na Serikali ya Regional Assemblies. Hii itachangia katika kuleta huduma za kiserikali karibu na wananchi zaidi. Pia inamwezesha wananchi katika sehemu yeyote ya Kenya kushiriki kikamilifu katika maendeleo, yawe ya Serikali, ya Uchumi hata Elimu. Kwa sababu tunavyoona sasa - nataka mniruhusu nitoe mifano kidogo kidogo tu.

**Com. Asiyo**: Lakini kwa muda mfupi sana - kupendekeza ndio kitu ya maana.

**Kalama Alphonce John:** Tuangalie Uchumi. Hapa kuna wakati mmoja kulikuwa na kiwanda cha Maziwa, hapa Mariakani tu. Na, kuna research hapa nchini ya kilimo, Mtwapa, badaye ikafwatiwa na chuo cha Ukulima Kilifi. Angaliene vile ilivyofanyika! Hiki kiwanda cha maziwa kikafilizika; kule, chuo cha ukulima kikiinuka, kiwanda cha Kurosho kikafilizika. Wakati huo huo, chuo cha sukari hapo chini Ramisi kikafilizika - na hali research iko hapa hapa Mwatapa. Hivi sasa ukitega sikio na ukitembea katika nchi yetu utasikia Sony Sugar, Mumias - tunashangaa Unitary Government ilikuwa ina panga vipi vyuo hivi na ma-reaserch haya, na tena huku viwanda vile vile ambavyo vingekuwa vinakuwa supported na kuwa extended na vyuo hivi vinaanguka? - Kulikuwa na upendeleo.

Ya pili tuangalie umilikaji wa ardhi. Nitatoa mfano hapa kwa kuwa hapa ndipo nimezaliwa na nimekulia hapa zijaenda nje sana kwa wenzetu - lakini ninasoma na pia ninasikia. Kwa wenzetu ardhi imegawanywa - I mean, adjudicated na watu wamepewa Title-deeds ili kuwasaidia kupata mikopo. Leo, hapa kwetu tokea tupate uhuru, kuna sehemu kubwa haijafanyiwa shuhuri hiyo. Kuna watu wamekaa nchi ya mtu ambaye hivi sasa anaweza kuwa yuko Ulaya ama nchi zingine za nje - hausiki. Squatter tu, squatter kila siku. Isitoshe hiyo wenzetu wana mamlaka ya kuja na karatsi na kukuonyesha - "Eh Bwana we" - anakuonyesha puani kabisa anakwambia "We unaiona karatasi hii, hapa ni kwangu hapa" - Ameipata Nairobi. Unashangaa kizazi changu chote, umri huu niliofika mimi hata nikiwa ni mtoto, lakini si inatosha kabisa ya kwamba pale nilipo ni kwetu. Unaonyeshwa karatsi ya kwamba mtu amepata karatsi hiyo ya kumiliki ardhi ile anayo. Ningependekeza hivi; ule uwezo wa Commissioner of Lands tuupunguze. Haya mamlaka ya mashamba yapelekwe kwa Regional Assemblies.

La mwisho: Katika Armed Forces; na nikizungumzia Armed Forces nazungumzia Kenya Army, Air Force na Navy - tunapendekeza ikifika wakati wa recruitment ikiwa haitawezekana kupata vijana sawa sawa kutoka kila sehemu; na kila sehemu nina maana ya kusema kila jimbo, basi hii quota system ifanye kazi. Na iwe quota system ambayo inaeleweka, recruitment ya Armed Forces hizi tatu ieleweke hivyo. North Eastern ikiwa kuna recruitment wawe na quota yao - huo natoa kama mfano tu - wawe na quota yao vijana kadha waingie Armed Forces. Isiwe hivi; wenzetu wa North Eastern mnawajua na nikizungumza ndugu, wa kutoka Nyanza tunawajua, nikizungumza ndugu wa kutoka Central tunawajua, si ndio? Asiwe ni mtu anatoka North Eastern na ukimwangalia hali zake anatoka Central Province. Utakuwa uwalikisha North Eastern katika recruitment hii. Polisi

wawachwe tu katika regional assemblies or regional - whatever we shall call them. I mean to stay kila region iwe na polisi wake kulinda tu. Kumekuwa na kilio cha Bwana mmoja aliyetangulia hapa, na ni kweli kabisa, nitawapa mfano, mama wa hapa …………

**Com. Asiyo:** Moja tu, dakika moja ………….

**Kalama Alphonce John:** Mama wa hapa nikisema wa hapa - Giriama, Mrabai atatoka na ndundu la wine ya mnazi nyinyi mnaita pombe ni wine, atoke nayo hapo, akitoka barabarani, ama kama vile mwenzangu alivyosema hapa, anafutwa nyumbani kabisa, anafanyiwa msako. Vile ya kwamba ni awe na ruhusa –A- ah- anambiwa, "we twende". Lakini angalia polisi; polisi anatoka wapi? Polisi yule anatoka wapi? Kunatoka mama kule Mombasa anakuja Rabai ama Kaloleni kuchukuwa wine ile ile ya mnazi na atatia kwenye gari "Vroom" - itafika Mombasa na watu watakunywa daily bila kuguzwa; kwa kuwa mama yule si yule Kadhi ama Kaswa ama sijui nani. Hii tunataka tuiharamishe. Wananchi waruhusiwe kutumia rasilmali zao vili inavyositahili. Hata nikependekeza, mwape ruhusa wakate licence za kuendesha hiyo. Asanteni sana.

**Com. Asiyo:** Tumeshukuru sana Bwana Kalama …………………(inaudible).

**Com. Leneola:** …….(inaudible) Useme mapendekezo yetu ni kazi ya ……. .(inaudible) tujue pendekezo lako ile jimbo iwe ni ya wapi katika Mkoa, Wilaya

**Kalama Alphonce John:** Liwe jimbo, serikali ya jimbo iwe katika ngazi ya Mkoa

**Com. Leneola:** Ya mkoa, na unataka wandike polisi wao wenyewe?

**Kalama Alphonce John:** Polisi wao wenyewe.

**Com. Asiyo:** Wengine sasa hutaki………….

**Kalama Alphonce John:** Polisi.

**Com. Asiyo:** Ma-chief?

**Kalama Alphonce John:** Ma-chief si necessary. Kikosi kingine ambacho nilikuwa umenikumbusha mama - nataka niombe kiondolewe ni hii National Youth Service. Sijui kama mnaiona maana lakini naona ni …………………..

**Com. Asiyo:** Maoni yako …………………………………….

**Kalama Alphonce John:** Maoni yangu ni kwamba ni gharama kwa raia.

**Com. Asiyo:** Asante. Sasa tuko na Bwana Hassan Salim ningeomba sana kina mama pia tafadhali mhudhurie na muweze kuongea mawazo yenu. Ni kitu cha muhimu. Mtupatie mawaidha yenu…….

**Hassan Salim:** Commissioner na wageni mlioko hapa ninafurahi kupata nafasi hii, mimi jina ninaitwa Hassan Salim mfanyi biashara. Kusema kweli, nachangia meneno ambayo nitayazungumzia hapa kwa ajili ya Katiba tunayotaka. Maoni yangu ni kuwa; Serikali tuliyo nayo sasa tunaona inaenda kimakosa, kwa sababu ya mamlaka ambayo wamechukuwa kubwa sana. Kwa upande wa Rais………………………

**Com. Leneola:** Pendekeza.

**Hassan Salim:** Mapendekezo: Kuwa Rais amepewa jukumu kubwa sana ambalo hawezi kulibeba. Kwa sababu yeye ndiye Mkuu wa Majeshi, yeye ndiye "above the law", yeye ndiye tu anayechagua Ministers mpaka kazi hizo zote, ndio unakuta ufisadi unatokea pale. Maana ya kusema hivyo ni kuwa Rais akiwa ni above the law, tunaweza kupata Rais ambaye ni mwizi - hatuwezi kumushtaki. Tunaweza kupata Rais muuaji hatuwezi kumushtaki, kwa hivyo mamlaka kama yale yaondolewe.

Jambo la pili ni kuwa yeye anachagua Ministers. Ili jukumu la kuchagua Minister ingekuwa bora ni Bunge lenyewe liwachague. Kwa sababu ya kusema hivyo ni kuwa yeye ikiwa ni kabila fulani, ni lazima yeye atachagua kabila yake kwanza kujaza zile ministries na hivyo ndivyo inavyokuwa. Na ndipo hapo ukakuta watu wanapiga kelele "Ukabila upo". Na jambo la pili ni kuwa hizi political parties - zimekuwa nyingi Kenya. Ningependelea maoni yangu kuwa ziwe kama tatu nne – visiwe sitini. Sababu yale mengi huwa ni watu binafsi wanatia zile pingamizi za vyama vingine. Tena hizi political parties, hatujui ni nani ata-finance; lazima ile finance itatoka kwa nani - kwa Serikali, kwa watu binafsi au party yeyewe?

**Com. Lethome:** Pendekezo, unataka namna gani?

**Hassan Salim:** Mimi naona afadhali kama ni political party kila mmoja asitegemee pesa za Serikali. Uhuru wa mahakama; Napendekeza mahakama iwe huru, kuwe na kamati ya mahakama ambayo wao watachagua ma-judge wenyewe wa mahakama.

Local Government Authority; hii wizara huwa ni wizari ambayo ni wananchi wameichagua-ma-Councillors, ma-Mayor. Pendekezo langu ni kuwa Councillors lazima wachaguliwe na wananchi na wawe na elimu ya form four. Tusibandikiwe watu ambao hawaelewi kusoma na kuwandika. Na pili tusiwe na ma-Councillors ambao wamefanyiwa nomination, hatuna haja na nominated, sababu hakuna kitu wanatufanyia. Hapo hapo katika Local Government tunakuta upande wa Land; land lazima iwe chini ya Local Government na iwe na mashauri kutoka wenyeji wa sehemu ile. Wanapotangaza ardhi au kutaka kutoa ardhi kwa mtu yeyote, kuwe na matangazo ambayo wananchi wa pale wataelewa. Sio watu kutoka nje wanakuja kunyakuwa ardhi

zetu na sisi tuko pale.

Enivornment na regional natural resources; Enivornment lazima iangaliwe katika sehemu ambayo tuko; sio mtu atakuja kuweka viwanda ambazo zitadhuru maisha ya binadamu kwa sababu tu kuwa kiongozi fulani anapewa kitu fulani inapitishwa. Kwa hivyo lazima wananchi wahusishwe. Natural Resoures ni kama ardhi ambayo iko na madini. Tuchukue mfano, ni kama ile ya Kwale Titanium - imekuja kunyakuliwa wananchi hawajui. Kwa hivyo kitu kama kile kitaleta uhusiano mbaya na kuchukia serikali kutoka kwa wananchi. Ni hayo tu.

**Com. Asiyo:** Asante sana Bwana Salim.

**Com. Leneola:** Subiri kidogo ……….(inaudible) hivi vyama vy kisiasa vilivyosajiliwa ni arubaini na sita au arubaini na saba. Sasa tufanye nini, tutatumia criteria ipi ili kupunguza mpaka tubaki na hivi vitatu au vine?

**Hassan Salim:** Hiyo ni waambiwe wachukue maoni ya wananchi - wapate at least 50% kutoka kwa wananchi.

**Com. Leneola:** Kama kura ya moani?

**Hassan Salim:** Kura ya maoni ndio.
**Com. Leneola:** Referendum.

**Com. Asiyo:** Umemaliza? Asante nenda ujiandikishe pale kwa register yetu. Bwana Kambi Mjomba tafadhali, Bwana Kambi Mjomba.

**Kambi Mjomba:** Salamu aleikum.

**Com. Asiyo:** Hebu tueleze jina lako kwanza.

**Kambi Mjomba:** Naitwa Kambi Mjomba.

**Com. Asiyo:** Kambi Mjomba asante endelea.

**Kambi Mjomba:** Nimeshukuru kwa kunipa nafasi hii, kwanza, mimi ni mzee nimezaliwa 1939. Na sasa inaonekana ya kwamba ni serikali hii iliyoko sasa ……………..(inaudible) Nikizungumza hivi ya kwamba, hapa nipo, huyu Bi Matembo unambiwa - hii tembo ukinywa unambiwa imefanya makosa.

**Com. Asiyo:** Wewe tueleze mapendekezo yako juu ya pombe hii.

**Kambi Mjomba:** Juu ya pombe ninasema kwamba, hivi niko hapa nimefungwa mwaka mmoja kwa ajili ya mnazi. Na zamani kulikuwa hakuna hiyo wakati wa mkoloni. Mkoloni alikuwa anawachilia uhuru ama anakufunga siku moja.

**Com. Leneola:** Sasa ungependa katika Katiba mpya ufungwe siku ngapi?

**(Laughter from the audience)**

**Kambi Mjomba:** Sitaki kufungwa siku zozote.

**Com. Leneola:** Hutaki kufungwa?

**Com. Asiyo:** Kila siku?

**Kambi Mjomba:** Kila siku mpaka nimalize mwaka mpaka mwaka ujao mwezi wa tatu

**Com. Leneola:** Endelea.

**Kambi Mjomba:** Sasa nazungumza hivi; kama Katiba mpya ikiwa itaondoa maovu haya yote, maanake wakati wa zamani wakati wa mkoloni kulikuwa hakuna.

**Com. Leneola:** Maovu kama yapi - number moja mfano?

**Kambi Mjomba:** Uovu kama Serikali ya sasa ya Nyayo.

**Com. Leneola:** Kwa mfano toa mfano mmoja.

**Com. Asiyo:** Toa mfano.

**Kambi Mjomba:** Mfano mmoja ni kwamba sasa wewe ukilewa unaambiwa “drunkard and disorderly”.

**Com. Leneola:** Sasa pendekezo, ungetaka ukilewa uaambiwe nini pendekezo?

**Com. Asiyo:** Ukilewa ufanyiwe aje uzaidiwe nyumbani?

**Kambi Mjomba:** Eh niende nyumbani.

**Com. Leneola:** Haya asante.

**Com. Asiyo:** Ingine tena.

**Kambi Mjomba**: Kwa nini leo ukilea …………………..

**Com. Leneola:** Jambo lingine?

**Kambi Mjomba:** Polisi, ukifika pale pia polisi – "sijui Katiba mpya ni kitu gani", wewe unawekwa ndani na wale polisi wa Kiganjo……………..

**Com. Asiyo:** Pendekezo lingine?

**Kambi Mjomba:** Pendekezo lingine ni kwamba tutanaka Rais mwengine ambaye anaweza kuondoa hii sheria.

**Com. Leneola:** Kwa mfano Rais awe na elimu ya kiwango gani?

**Kambi Mjomba:** Iwe ya juu hata kama ni kijana hata kama ni mzee.

**Com. Leneola:** Awe na umri wa miaka mingapi Rais?

**Kambi Mjomba:** Hata kama ni wa miaka thlathini.

**Com. Leneola:** Haya na chini na afikishe miaka mingapi?

**Kambi Mjomba:** Juu zaidi hata ikiwa miaka arubaini ama miaka mia tano.

**Com. Asiyo:** Ile ya mwisho kabisa juu zaidi ni ngapi?

**Kambi Mjomba:** Juu zaidi itakuwa forty ama forty-eight.

**Com. Asiyo:** Halafu, mtu wa miaka hamsini hawezi kuchaguliwa kuwa Rais?

**Kambi Mjomba:** Anachaguliwa kwa nini?

**Com. Leneola:** Na miaka tisaini?

**Kambi Mjomba:** Tesaini amekuwa mzee.

**Audience:** (Laughter)

**Com. Leneola:** Na themanini?

**Kambi Mjomba:** Themanini hiyo hapana.

**Com. Leneola:** Sabini na tano?

**Kambi Mjomba:** Ni sawa tu.

**Com. Leneola:** Okay mpaka Sabini na tano – isipitishe hapo?

**Kambi Mjomba:** Asipitishe hapo.

**Com. Leneola:** Na elimu yake umesema iwe kiwango gani?

**Kambi Mjomba:** Hata kama ni form six hata kama ni form ngapi………lakini hata ……..

**Com. Leneola:** Na ungependa tuwe na Rais mwanamke?

**Kambi Mjomba:** Nataka Rais mwanamke pia - hata kulikuwa na Indra Gandhi kule India aliyekuwa yeye anaendesha Serikali.

**Com. Asiyo:** Haya sawa Bwana Kambi asante sana - tafadhali enda pale uweke jina lako. Tumeshukuru sana; sasa Bwana Hassan.

**Com. Leneola:** Huyo ameshatoa maoni yake.

**Com. Asiyo:** Okay; Lawson Nzomo, Bilton Nzomo.

**Lawson Nzomo:** Niko hapa Commissioner. Asanteni sana Commissioners na wenzangu ambao mko hapa kuchangia haya mambo ya Katiba. Kwanza kwangu imekuwa shukrani kuu sana, kwa sababu wakati kama huu tumeulilia siku nyingi ambapo tutaweza kupata fursa ya kutoa moja mawili ambayo twaona yatatiza.

**Com. Asiyo:** Yaseme sasa.

**Lawson Nzomo:** Na haya ni kama sasa - kwanza tunaanza na hii Local Authorities. Local Authorities ziko karibu na wananchi na zimekuwa mzigo kwa mwananchi. Kwa sababu Local Authorities zile hutumika kuidhinisha mashamba za watu bila wale walioko kwa hiyo hiyo ardhi kuhusika. Tukirudi hapo, baada ya uchaguzi wa hizi Local Authorities uwa kuna uchaguzi mwingine ule wa Mayor ama mwenyeviti. Kivyangu mimi ningependekeza mbele ya Tume hii kwamba, vile wanavyochaguliwa wale Madiwani, wale ma-Mayor pia wachaguliwe vile vile. Kwa sababu, itakuwa ni rahisi kulaghai watu watatu, wanne mtu kunyakuwa kile kiti cha juu, ili kuweza kufanya mambo yake. Lakini ikirudi kule kwa watu, watu watachumbua, "eh sasa imefika wakati wa Mayor". Mayor anahitajika awe kivipi? Watachumbua wajue yule ambaye anafaa wadhifa ule aweze kuubeba. Tukirudi hapo, tunarudi katika mambo ya kupiga kura. Kupiga kura imekuwa ni haki ya kila mtu na mara nyingi huwa inakumbwa na undanganyifu mwingi.

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo sasa tufanye je? Unapendekezo gani?

**Lawson Nzomo:** Ninavyopendekeza mimi, baada ya zile kura kupigwa, sihesabiwe palepale kwa kituo. Tukirudi hapo………………………….

**Com. Asiyo:** Uko na dakika mbili Bwana Nzomo.

**Lawson Nzomo:** Tukirudi hapo tuko kwenye hizi political parties. Political parties ambazo ziko sasa katika jamhuri yetu mara nyingi zimeundwa kwa misingi ya watu kutengeleza masilahi za watu binafsi hazina mandate ya wale wananchi kwamba wamekubali chama hii ikaanzizwe. Sasa hivyo basi, inazifanya wakati wako katika mijandala yale ambayo yamuhusu wananchi wanapuunza ama kupinga na kupitisha yale ambayo yana faida kwao.

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo wapendekeza aje sasa?

**Lawson Nzomo:** Pendekezo ni kwamba hizo political parties ziwe zinapata maoni kama inataka kumbuniwa kutoka kwa watu. Ili wapate kujieleza na watu wapate kuwajua wenye kuunda hivi vyama ni wakina nani. Na labda hatutakosa mambo moja, mawili ambayo watuulizwa. Halafu ikishathibitiswa kwamba sasa kila mmoja ametosheka, nafikiri kutakuwa kuna go-ahead. Hata zile shida zitakuwa zikienda zinaenda na imani ya watu, kwa sababu ni chama ambacho wamekikubali na wanaelewa yale majukumu kitachoendesha.

**Com. Asiyo:** Asante sana; umemaliza sio?

**Lawson Nzomo:** Bado kidogo.

**Com. Leneola:** La mwisho.

**Com. Asiyo:** Liwe la mwisho tafadhali, tena fanya pendekezo tu.

**Lawson Nzomo:** Kuhusu mambo ya utawala - mfumo wa Serikali. Kivyangu mimi mfumo ambao ungefaa sasa nchi hii, basi ungalikuwa mfumo wa majimbo. Kwa sababu hii; Serikali ya umoja kama ilivyo sasa inaitajika kuwa na majukumu ya kuwangalia kila corner ni wapi pamezorota, ni wapi hapafaidiki lakini kufikia sasa ziko sehemu ambazo zimepuuzwa kimaendeleo, hazishughulikiwi kabisa, kama ambazo hazina watu. Lakini ikiwa siku watu wanataka yale masilahi yao ndio sasa wanakimbia mbio "njooni njooni". Ikipita il masihali, wamesauliwa. Kwa hivyo nafikiri hayo ndiyo yale machache ambayo ningechangia.

**Com. Leneola:** Hii Jimbo unataka liwe katika sehemu gani?

**Com. Asiyo:** Kwa Province au kwa District au wapi?

**Lawson Nzomo:** Kwa Province.

**Com. Leneola:** Watu wanalalamika kuwa ma-chief …………………(inaudible).

**Lawson Nzomo:** Mimi nafikiria hapo katika fikira hizo, nafikiri hizo zitakuwa zimetafautiana na zangu. Kwa sababu ninavyojua mimi, tuko na mkoa minane. Na kila mkoa utakuwa una mambo yake ambayo wanapanga pale na kupitisha na kutekeleza pale. Sasa sioni kama ule ukabila utatoka wapi, kwa sababu kitu ambacho tunatafuta katika hiyo ni kwamba ile huduma iwezi kumfikia yule mwananchi wa chini kabisa kule. Kwa sababu ikiaanzia national level, itakwamia kwa district, kule kwa mitaa haitafika.

**Com. Asiyo:** Tumeshukuru sana Bwana Lawson, tafadhali nenda pale ujiandikishe kwa register yetu. Bwana Sudi Ngala, Sudi Ngala karibu. Karibu sana mwenzangu ukae hapo chini, ukitaka kusimama ni sawa, kisha utuelezee majina yako yaingiee kwenye hii machine.

**Sudi Ngala:** Kwa jina naitwa Sudi Ngala mfanyi biashara hapa Mariakani. Mimi naoni yangu ni kuhusu Kenya - vijana wengi

hawana kazi na wanalia kila siku. Na utakuta Serikali mtu alikuwa mkubwa mfano kama Raru Raru alikuwa mkuu wa majeshi, ame-retire amerejeshwa tena Chairman wa KPA. Sasa utakuta umasikini unazidi kuendelea watu hawana kazi. Na vijana wanaendelea kusoma na kumaliza hakuna kazi kwa sababu mtu akiwa mkubwa, akisha retire anaondolewa anaekwa mahali pengine.

**Com. Leneola:** Pendekezo, hao walio-retire tuwafanye aje?

**Sudi Ngala:** Pendekezo langu ni kuwa mtu akisha retire arudi nyumbani akakae atulie ili vijana wengeni nao wapate kupata nafasi.

**Com. Leneola**: Na lingine?

**Sudi Ngala:** Lingine ni kuhusu land.

**Com. Asiyo:** Kuhusu land – ardhi?

Sudi **Ngala:** Utakuta ma-squatter wengi sana hapa Kenya; Mtu amekaa kwa miaka hamsini - babu yake, babu yake, babu ya babu yake wamezikwa hapo, halafu baada ya muda kuna kuja mtu anatoa Title-deed amasema hapo ni kwake, kwa sababu yeye ana pesa.

**Com. Leneola:** Pendekezo?

**Com. Asiyo:** Pendekeza sasa tufanye aje?

**Sudi Ngala:** Pendekezo langu ni kuwa Katiba ijayo, iwe mtu kama pale mahali kumechuguzwa ni kwake, kuwe hakuna haja ya mtu akija na title-deed iwe hawezi kupachukua.
Ni hayo tu.

**Com. Asiyo:** Kwa miaka mingapi?

**Sudi Ngala:** Kama miaka mitano hivi**.**

**Com. Leneola:** Na umeiishi mahali miaka mitano………..

**Speaker:** Miaka mitano ni kidogo sana.

**Com. Leneola:** Maoni yake hayo maoni yake yaheshimiwe. Asante Bwana Ngala.

**Com. Asiyo:** Okay sasa tuko na Antony Jambo mfanyi biashara hapa karibu

**Antony Jambo:** Mimi naitwa Antony Jambo. Pendekezo langu ni kwamba Rais awe chini ya sheria.

**Com. Asiyo:** Endelea.

**Antony Jambo:** Serikali iwe ya Majimbo. Mayors na wenyeviti wachanguliwe na wananchi.

**Com. Leneola:** Mayor na Chairman?

**Antony Jambo:** Ma-chairmen wachaguliwe na wananchi.

**Com. Asiyo:** …………………(Inaudible)

**Antony Jambo:** Wananchi kwa miaka mitano.

**Com. Asiyo:** Wachaguliwe na watu?

**Antony Jambo:** Ndio. Madiwani wawe masomo yao ni daraza la nane, isiwe juu ya hiyo.

**Com. Asiyo:** Akiwa amefika form four?

**Antony Jambo:** Akiwa form four basi aingie akishindana na yule wa nane. Sioni uoga uko wapi. Si wewe utaelezea habari ya masomo yako? President awe ni wa form four na kuendelea, kwa sababu sioni kama kuna uoga wowote wale wame graduate wanaogopa. Kwa sababu wewe kama ni graduate, wananchi watakuwangalia na wakupitishe - wakitaka kama wewe ni mzuri kuziwe na kiwango chochote.

Okay, 25% izuiwe kutokana na kuna katika Kenya una mkabila mengine yanatosha kabisa kuchukuwa hiki kiti bila ongezeko la mtu yeyote na hiyo itakuwa hatari kwa majimbo mengine.

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo ifanyawe aje?

**Antony Jambo:** 25% iendelee kubaki kwa Mikoa mitano

**Com. Asiyo:** 25% kwa kila Mkoa.

**Antony Jambo:** Kwa Mikoa mitano, President akishinda, hata kura ziwe kidogo namna gani, ameshida kwa hivyo aende.

**Com. Lenaola:** Hata kama kidogo namna gani?

**Antony Jambo:** Akishinda hata kama ameshinda kwa elfu kumi ni sawa wacha aende. Kwa sababu hii nchi haiwezi kuhudumia uchaguzi mara mbili kulingana na hizo percentage tumeweka. Sina nyingine zaidi.

**Com. Leneola:** Majimbo katika ngazi gani?

**Antony Jambo:** Katika ngazi za Mkoa.

**Com. Lenaola:** Tungependa mtu yeyote ambaye ana maoni, ama anapendekeza ya majimbo atuambie …………….(inaudible)

**Com. Asiyo:**…………………(inaudible)

**Antony Jambo:** Mimi napendekeza ya mikoa.

**Com. Lenaola:** Na ungetaka MP awe na masomo gani?

**Antony Jambo:** Masomo ya form four. Isipokuwa kukiwa na graduate, aingie uwanjani; anaogopa nini uoga uko wapi na yule hajasoma? Wewe umesoma elezea kusoma kwako.

**Com. Asiyo:** lazima ujiandikishe pale kwa register yetu na tumeshukuru sana kwa maoni yako. Sasa twaenda kwa Hamisi Mweni.

**Hamisi Mweni:** Asante sana Makamishina wa Tume na wananchi wenzangu mliohudhuria. Jina langu ninaitwa Hamisi Mweni. Mapendekezo yangu kuhusu mfumo wa utawala, napendekeza mfumo wa Majimbo, katika kiwango cha Mkoa. Katika mfumo ule wa Majimbo pendekezo langu, utwala wa Mikoa siuhitaji. Labda kungepangwa watu kama Makatibu kutoka mkoani, Wilaya, Tarafa hata mpaka Kata ndogo ikiwa ni Sub-location

**Com. Asiyo:** Makatibu?

**Hamisi Mweni:** Ndio; ku-represent Utawala wa Mikoa.
Kuhusu elimu ya Madiwani, napendekeza darasa la nane. Sababu zangu ni kwamba sehemu ninazotoka kuna kwingine ambako hata wale wa darasa la nane wako ni wachache, wale wa form four pengine wanaweza kukosa kabisa. Na vile ninavyo elewa mimi ni kwamba kwa huu mfumo yule diwani ni lazima atoke sehemu ile. Sijui tukiweka kiwango cha form four na kuendelea atatoka upande gani ili aje awakilishe ile sehemu.

**(Clapping)**

**Com. Lenaola:** Endelea.
**Hamisi Mweni:** Kuhusu uchaguzi wa madiwani na wenye viti ningetaka wachaguliwe moja kwa moja kupitia kwa wananchi.

**Com. Asiyo:** Hao ni ma-mayor au……….

**Hamisi Mweni:** Madiwani na wenyewe viti mabaraza na ma-mayor. Saa hii sina mengi ya kuongeza, niko na memorandum ambayo nitaikabithi. Hiyo ndio nimeandika kila kitu. Asanteni

**Com. Lenaola:** Swali tu moja. Umesema hawa makatibu wachaguliwe kutoka kwa PC, DC, DO hata kwa Assitant-Chief - tukuwe na makatibu kutoka chini mpaka juu.

**Hamisi Mweni:** Ku-represent ule utawala wa Mikoa iliyoko sasa.

**Com. Lethome:** Watachaguliwa, hao Makatibu wachaguliwe na nani?

**Com. Asiyo:** Nani atakaye wachagua?

**Hamisi Mweni:** Wateuliwe na hilo Bunge la jimbo.

**Com. Asiyo:** Wateuliwe na hilo bunge la Jimbo au………………

**Hamisi Mweni:** Wateuliwe na hilo Bunge la Jimbo. Kama kuna swali lingeni niko tayari.

**Com. Asiyo:** Sasa Bwana, wewe umemaliza. Tuko na J. G. Nguma.

**J. G. Nguma:** Niko hapa.

**Com. Asiyo:** Asante. Karibu.

**J. G. Nguma:** Okay mapendekezo yangu ni haya.

**Com. Lethome:** Majina kwanza.

**Com. Asiyo:** Majina kwanza

**J. G. Nguma:** Jina langu ni J. G. Nguma. Lile ambalo nimeandika hapo. Mapendekezo yangu ndio haya. Serikali yenyewe iwe Serikali ya Majimbo. Na Serikali hii ya Majimbo iwe kwa ngazi ya Mkoa. Na ikiwa katika ngazi za Mkoa, iwe na Bunge na Kiongozi wa hilo Jimbo ambaye ana mamlaka zaidi. Hii nikumaanisha kwamba Rais wa kitaifa hatakuwa na mamlaka – mamlaka yatakuwa na viongozi wa Majimbo. Na katika uongozi huu wa Majimbo, Serikali za wilaya ziendelee kudumishwa, lakini ma-Mayor na wenye - viti wachaguliwe na wananchi. Na Katiba katika Serikali hizo za Wilaya aidhinishwe na Serikali ya Jimbo. Na vile vile katika upande wa utawala wa Mikoa, Ma-chief pamoja na ma-Assistant Chief wachaguliwe na wananchi. Na wale ambao watakuwa katika ngazi ya Tarafa na Wilaya, waidhinishwe na Serikali ile ya Jimbo.

Tukitoka hapo naenda kwa rasilmali hii ambayo ni ardhi - Commissioner wa ardhi ambaye anakaa katika ngazi ya ki-taifa awe na mwakilishi katika kila Jimbo. Na mwakilishi huyu atakuwa akikaa na viongozi wa Jimbo na kuidhinisha mambo yote ya ardhi katika Jimbo. Commissioner mwenyewe kule abaki kama Rubber-stamp peke yake.

Tukienda kwa upande wa uhuru wa mahakama; Jimbo, katika mijadala ya Jimbo I-idhinishwe mambo ya ki-Katiba ambayo, au tuseme kwamba mahakama ipatiwe uwezo wakuwa huru kabisa. Wafanye kazi bila kuingiliwa. Wakati wakiwa wamechaguliwa basi kwa vipindi vyao wawe wanafanya kazi bila kuingiliwa na mtu yeyote.

Tukitoka hapo nataka ningie katika upande wa elimu – Katika upande wa elimu, kila jimbo liwe na shule za ki-taifa - National Schools. Maana saa hii concentration iko upande mmoja, kuna sehemu zingine ambazo hakuna hata moja kabisa. At least kuwe na kama two national schools katika kila Jimbo au hata zaidi. Na katika National Schools hizi, zidumishe hali ambapo kutakuwa kuna wanafunzi kama ni a quarter, wanachaguliwa katika Taifa na ¾ wanatoka katika ili Jimbo, lile kuimarisha hali ya elimu upande huo.

Tukienda kwa vyama; hivi vyama vya kisiasa – Ili chama cha kisiasa kiweze kubuniwa kuwe na kura ya maoni na at least chama hicho kipate at least 30% katika hiyo kura ya maoni. Basi hapo kinaweza kuwa chama, kuliko vile hali ilivyo ambavyo hata mimi nikiwa niko tajiri naweza nikaazisha chama changu.

**Com. Lenaola:** ………..(Inaudible) Bwana, eh……………………..

**J. G. Nguma:** Bwana Nguma; niendelee?

**Com. Asiyo:** Endelea tu.

**J.G.Nguma:** Kitu kingine ambacho ninataka kuzungumzia ni mambo ya ufisadi ambayo yamechukuwa nafasi kubwa sana katika kuzorotesha uchumi wa nchi. Ninapendekeza kwamba watu ambao watakuwa katika mamlaka na ambaye atapatikana kwamba amefanya mambo ya ufisadi, Katiba itoe kifungo ambacho kitakuwa kinajulikana ambacho ni kikubwa zaidi - hata kama ni miaka ishirini. Na mtu ambaye amejulikana, pengine anachuguzwa ameonekana kwamba kuna mambo ya ufisadi ambayo anafanya na yuko katika uchunguzwa, ikiwa yuko katika mamlaka ya umma asimamiswe.

Kuna utumishi wa mamlaka; kuna watu ambao pengine wamepatiwa mamlaka makubwa katika Serikali na wanatumia mamlaka yao kunyanyasa watu wengine. Huo uchukuliwe kuwa ufisadi hivyo hivyo; na yeyote ambaye atapatikana katika hali kama hizo, basi kuwe na kifungo ambacho hakipungui maika kumi kuendelea.

Halafu kuna utumishi wa umma – Katika utumishi wa umma, file zote za watumishi wa Serikali ziko Nairobi kwa wakati huu, ambapo mtu akiwa na matatizo, wengeni hata hawajui Nairobi inakuwa shida, kwa hivyo anambaki na matatizo yake kwa muda huo wote. Kwa hivyo sasa, file zote za utumishi wa umma zirudi kwa ngazi ya Jimbo ambako itakuwa ni rahisi kwa mtu ambaye yuko na matatizo kwenda na kupata hiyo huduma kurekebisha matatizo yake huko.

Uchaguzi; Ile hali ya 25% ya uchaguzi wa Rais indelee kudumizwa. Yaani Rais awe kwamba anapata at least 25% ya votes in five Provinces. Na halafu kuna maswali ya jinsia ambapo tumekuwa tukisikia watu wengine wakisema kwamba kuteuliwe akina mama wapatiwe viti katika Parliament bila kuvipigania. Huo utakuwa si usawa - vile ambavyo siku hizi utakuta kwamba hata watoto wa shule, unasika kwamba katika shule yetu hapa, aliyekuwa number one katika hiyo shule mtihani wa darasa la nane ni mwanamke - ni msichana tuseme. Msichana huyu amefanya bidii na ndio akapata ile nafasi. Kwa hivyo akina mama wajitokeze na wapiganie viti sawa na waume. Atakaye pita na akiwa na kiwango kizuri cha elimu, atachaguliwa kuwa Waziri- kama ana degree yeye atachaguliwa kuwa Waziri. Lakini sio mtu afanye kupatiwa kiti ambacho hakukipigania hatakitumia vilivyo na itakuwa tunaweka watu ambao wanakula mishahara mikubwa ya Serikali na hukana kazi yeyote ambayo inaendelea kule. Nitaachia hapo.

**Com. Asiyo:** Asante sana. Swali moja tu.

**Com. Lethome:** Umezungumza habari ya Mahakama iwe na uhuru lakini tunajua mara nyingi uhuru wa kitu chochote,

utategemea ule uteuzi nani anayeteua. Ningependa sasa upendekeze Judge Mkuu na Ma-judge wengine watauliwe na nani? Kwa sasa wanateuliwa na Rais siku za usoni ungependa wateuliwe na nani?

**J. G. Nguma:** Ningetaka kwamba kuwe na majadiliano ambako pengine Bunge itapitisha na ikipitisha Rais apatiwe majina ya watu ambao wameonekana kwamba wana-qualify, basi ateuwe mmoja katika wale ambao atakuwa amepatiwa.

**Com. Asiyo:** Swala lingine. Kwa ajili ya vile elimu na mambo ya kikabila yamezuia wasichana au kinamama kupata masomo zaidi kwa siku zilizopita. Nchi zingine za Africa zimeonelea ni vizuri kina mama wapewe nafasi ya kungombea viti vyao. Kama vile Uganda inafanya, wanawake wakijitokeza kwa kila Distrcit halafu kunakuwa na election yao wenyewe. Yaani kama hapa Kenya, kila party itatoa mama mmoja kwenda kwa kila District, yule atakayechaguliwa kwa hiyo party, ndiye atakuwa Mjumbe wa hiyo Bunge. Halafu baadaye kutakuwa sasa na election ile ya kawaida - ambako wanaweka walio na nguvu - kama mimi nilikuwa Karachuonyo wanaweza sasa kusimama na akina baba hawachaguliwi. Hatusemi kwamba kina mama wapewe nafasi ya kuingia bila kufanyiwa uchaguzi; je kwa maana hawapatiwi viti vya bure, bado ungependelea tu kwamba wasipewe nafasi ya kusimama kwa viti vyao wenyewe, wachaguliwe na watu wao?

**J. G. Nguma:** Okay, mapendekezo yangu ni haya. Hata katika Serikai ya sasa wakina mama hawajanyimwa nafasi ya kupigania viti; kile kilichoko ni kwamba hizia za kiutamaduni ambazo zimetufunga, ndizo ambazo zinafanya wakina mama wanabaki nyuma. Kwa sababu ya hizo hizia za kiutamaduni ambazo sasa hizi, wale wote - pengine Katiba iseme kwamba wale wote ambao watachaguliwa katika mamlaka, katika Serikali za Majimbo, utumishi wa umma, Rais wawe mstari wa mbele katika kupiga vita hizia za kiutamaduni ambazo zimepitwa na wakati. Maana ikiwa utampatia mama yaani ili hali ya kutetea kwamba “upatiwe” hutatumia kikamilivu vile inavyohitajika; lakini kama umekipigania kama vile wasichana wetu katika shule ambazo wamechanganikana na wavulana, na utasikia kwamba, yule ambaye amekuwa wa kwanza katika Kenya nzima ni msichana au amekuwa wa pili, si uwa amepigania?

**Com. Asiyo:** Tunafahamu hiyo

**J. G. Nguma:** Basi iwe hali hiyo hiyo

**Com. Asiyo:** Asante sana Bwana Nguma hebu nenda pale ujiandikishe kwa register yetu. Sasa tuko na mama Bakarii jina lako ndilo la kwanza katika………..kaa nchini utueleze majina yako kamili halafu uanze.

**Pato Bakari:** Jina yangu naitwa Pato Bakari.

**Com. Asiyo:** Ongea tu.

**Pato Bakari:** Shida yangu ambayo imenifanya nije hapa kwa Commission hii ya Urekebishaji Katiba ni upande wa kina mama na wasichana wetu. Wasichana wetu, power imepewa vijana. Kijana atamtafuta msichana atamkatizia masomo na atampa mimba - hakuna njia utachukuwa hatua kwa yule kijana aweze kuzaidia yule mtoto; hiyo kina mama bado tunagadamizwa.

Na la pili, sisi wenyewe kina mama tumewekwa sana nyuma - sijui ni Serikali imetusahau au ni sisi wenyewe tumejiacha nyuma - kila tukikaa hasa kina mama ambao hatuna kazi za kufanya ni kazi tu ya nyumbani, kina baba hawatutambui. Utakaa na baba na baada ya muda pengine atapata bibi mwingine, na umepata na yeye mali fulani, hakuna msimamo wa kusema huyu mama amefanya bidii pia kwa jasho yake, hii mali pengine mama pia apate kidogo - unabakia tu hivyo. Kwa hivyo ningeomba maoni yangu, pia akina mama wanapoishi na kina baba wapate ile heshima ya kuwa ikiwa baba amefanya kichwa ngumu, pia mama aweze kupata share yake kwa ile jasho yake amefanya.

Kwa sababu akina mama ndio tunaochoka, baba pengine ataacha pesa, hana mpango wowote na hiyo pesa, mama utasema "nifanye hii kwa shamba, ninunue ka-ngo'mbe" lakini baada ya baba kupata mawazo mengine, itakuwa wewe mama sasa umeondokea patupu mwenye kutambuliwa ni yule ambaye atakuja halafu ataondoka bure. Pengine mama mimi nimezaa wasichana watupu, mwenzangu amekuja amezaa mtoto mmoja mvulana. Sasa mimi mama nitakuwa ninachunia yule ambaye amezaa vijana, yule mama ambaye ana wasichana, wasichana wake hawana urithi, kwa sababu ni wasichana. Ningeomba pendekezo langu, sheria hiyo kina mama pia upande wa urithi waangaliwe. Sina Mengi.

**Com. Lethome:** Mama swali. Vijana au waume wanaowatia watoto wa kike mimba ukependekeza wachukuliwe hatua gani?

**Pato Bakari:** Wachukuliwe hatua kijana……..Kwa sababu kina mama twasumbukana; nimelea watoto. tena mjukuu ataletwa, kijana ameaanza kuvaa ma-suit huko, wakikutana maneno ni mazuri, mama unasumbukana. Kwa hivyo kuwe kuna kiwango cha pia watoto wakizaliwa, family ya yule kijana alikotoka pia wapewe uzito wa yule mtoto aliyezaliwa na kijina wao.

**Com. Lethemo:** Kuhusu urithi mama, nitakuuliza swali moja. Umesema hapa katika urithi kuwe na usawa.

**Pato Bakari:** Usawa ninavyoomba au ninavyopendekeza – kama mama ataolowa awe ana bwana, wakati ule ile shuguli zote watakazo fanya, pia mama awe ana-power na kile walichofanya na bwana yake. Kama ni nyumba pia baba aheshimu mama, ajue mama ana share yake. Ikiwa wamefanya chochote iwe ni shamba, pia baba atambue kama mama pia ni nguzo moja kwa nyumba. Lakini kwa sasa hivi kina mama hatuna msimamo. Sasa utakuta hata mama anaona afadhali akauze Kaimati ajifanyiye mwenyewe kuliko kufanya na kutakuja kutokea mwenyewe. Kwa hivyo ningeomba kwa maoni yangu, hiyo sheria pia iwekwe chini tuangaliwe kina mama.

**(Clapping)**

**Com. Asiyo:** Asante sana mama Bakari kwa maoni hayo nenda pale ujiandikishe jina lako kwa register yetu. Sasa namuuliza

Bwana Francis Katana tueleze majina yako kikamili halafu uendelee.

**Francis Katana:** Mimi kwa jina naitwa Francis Katana.

**Com. Asiyo:** Haya endelea.

**Francis Katana:** Kwa upande wangu………………..

**Com. Asiyo:** Majina kwanza.

**Francis Katana:** Majina ninaitwa Francis …………………………

**Com. Lethome:** Sauti kidogo sauti.

**Com. Asiyo:** Sema kwa sauti ya juu.

**Francis Katana:** Kwa jina ninaitwa Francis Katana Gitau. Mimi ningependekeza hivi, katika hii Serikali ambayo tukonayo sasa ya ki-taifa, ningependekeza kwa muda wa baadaye tuwe na Serikali ya Majimbo. Na Serikali yenyewe ningependekeza iwe rahisi kutoka kwa Mikoa.

**Com. Asiyo:** Endelea.

**Francis Katana:** Na katika Mikoa hiyo, katika kila sehemu ya Mkoa, ningependa viongozi wa Mikoa wawe wakiteuliwa kutokana na baraza la Mkoa mwenyewe.

**Com. Asiyo:** Yaani viongozi wa…………………………

**Com. Lenaola:** Katika wale viongozi……………………

**Com. Asiyo:** Parliament. Tume ya Jimbo?

**Francis Katana:** Kuna lile Bunge ambalo litakuwa ni la Jimbo.

**Com. Asiyo:** …………….(inaudible)

**Francis Katana:** Kuuanzia yule Rais wa huo Mkoa.

**Com. Asiyo:** Endelea.

**Francis Katana:** Na kuna hawa tunaita Members of Parliament

**Com. Asiyo:** Si ni hao tu? Endelea endelea.

**Francis Katana:** Katika uchaguzi wa ma-diwani ningependelea Madiwani wawe na elimu ya kiwango cha standard eight. Na katika hawa tunaowaita Wabunge, ningependelea wawe watu wa kutoka kiwango cha form four na kuendelea. Singependa kuchangia mengi, yangu yalikuwa ni hayo machache.

**Com. Asiyo:** Asante sana Bwana Katana, sasa nende pale ujiandikishe halafu sasa tuko na Bwana James Kibwanga. James Kibwanga? Kama James Kibwanga hayuko………………….

**Audience:** Ndiye huyu.

**Com. Asiyo:** Tafadhali kuja mbele halafu useme majina yako kamili.

**James Kibwanga:** Majina kamili ni James Kibwanga. Mimi ninapinga Serikali ya U-rais na napendekeza Serikali ya Majimbo, kwa sababu Serikali ya U-rais inaonekana kulemeza wengine ambao hawana U-rais au hawako karibu na Rais. Kwa mfano, kwa sasa utakuta kila kabila ling'ang'ania U-rais kwa sababu wamejua kwenye U-rais kuna kufaidi. Sasa ikiwa namna hiyo, mimi Mgirima nikiwa Rais, basi Girima yangu itameremeta huko. Na Mkamba akiwa Rais, kule Ukambani kutameremeta kule. Kwa hivyo mimi nataka Majimbo kwa ngazi ya Mkoa.

**Com. Asiyo:** Sawa sawa endelea.

**James Kibwanga:** Upande wa afya, yako maswala mengi lakini mimi nitaguzia swala moja. Kuna maradhi fulani ambayo yanagadamiza watu - utakuta mtu ana ugonjwa mbaya ama mkubwa, mkali - tuchukulie hivyo - na anashindwa kujitibu.

**Com. Asiyo:** Kama AIDS?

**James Kibwanga:** AIDS, ama na zaidi - utakuta mtu anatakikana kuwa na kama laki tatu, laki nne ndio aende kujitibu. Na kwa sababu hana pesa hizo, anatezeka yule mgonjwa anafariki. Sasa mimi pendekezo langu katika Katiba hii itakayoundwa sasa, Serikali ichukue matatizo ya mgonjwa yeyote ambaye atashidwa kujitibu. Maanake tunaona kwa ma-TV wanaomba misaada kwa barabara, wanaomba misaada na ukiangalia wananchi wanateseka na Serikali iko - tu haijulikani Mbunge yuko wapi, Waziri wa afya yuko wapi. Kwa hivyo matatizo kama hayo Serikali ichukue siku za mbele.

**Com. Asiyo:** Endelea, endelea Bwana.

**James Kibwanga:** Upande wa Land, mimi napendekeza hivi: Ikiwa Serikali tumepitisha ni ya Majimbo, basi mngeni yeyote asiuziwe ardhi katika Jimbo. Ikiwa ana haja na ardhi akodishe. Kama atakodisha kwa miaka ishirini, atakodisha kwa miaka hamsini, kwa miaka tunajua 99 - lakini asiuziwe mtu yeyote ambaye si wa Jimbo hilo. Mtu yeyote ambaye si wa Jimbo hilo asiuziwe akodishe. Kwa mfano mitambo kama hii inavyokuja hapa. Badala ya kununua ama watu kusukumwa sukumwa, akodishe yule Mhindi ama yule mtu yeyote tajiri, akodishe kwa mwenye ardhi ili mwenye ardhi aendelee kupata rent ya mwaka, hata akifariki vizazi vyake viendelee kupata rent hiyo. Kwa hivyo badala ya kununua ardhi, wakodishe.

**James Kibwanga:** Na upande huo wa Lands, haya mambo ya kwenda Nairobi kutafuta title-deeds kwa vile tuko na Majimbo sasa, kila kitu kitakuwa kinaangaliwa hapa hapa kwa Mkoa. Maanake tumendanganywa sana; kuna mtu mmoja aliyesema anakwenda huko azungumuze kikabila yake huko, anatoa pesa yake fulani - tuseme huu kweli, "corruption hiyo"- anatoa pesa anakuja na karatasi hapa, anakwambia, "Ondoka Kibwanga, hapa ni kwangu". Na ukiangalia mimi hapa niko katika Mkoa wa Pwani kuna mtu ametoka Nyanza huko kwa kina mama Ogot huko anasema ni kwake. Katikati ya minazi anasema ni kwake! Inakuwaje hii? Unakuta Mgirima au Mijikenda anaondolewa chini ya minazi yake anakuja mama Ogot pale - haiwezekani. Kwa hivyo mambo ya title-deeds kule Nairobi, kwa vile tutakuwa tuna Majimbo sasa, na nina hakika tushayapata, eh! kila kitu itakuwa hapa hapa.

**(Clapping)**

Na upande huo huo wa Lands, kuna haya matatizo ya ki-familia, utakuta pengeni baba ana wake kama wawili, watatu hivi; unakuta akifariki yule mama mkubwa na watoto wake wanadai ile ardhi ni yao. Na yule bibi mdogo na watoto wake wanatengwa. Kwa hivyo hiyo Katiba ikiuundwa, iwekwe kwamba baba mwenye wanawake hata kama ni ishirini ile mali iwe ni yao - wagawanyiwe sawa sawa.

Upande wa, maswala ni mengi-wakati nao ndio huo upande wa elimu: Tukiambiwa kuna elimu ya bure iwe ni elimu ya bure. Kwa hivyo sasa kuna matatizo mengi unakuta inatangazwa na sheria imewekwa elimu ni ya bure lakini unakuta mtoto hana nguo rasmi za shule, hana uniform, hana vitabu. Elimu ya bure ni ile tu mshahara wa mwalimu lakini bado wazazi wanatezeka huko. Kwa hivyo ikitangazwa, ikiwekwa sheria elimu ya bure iwe ni ya bure mtoto atoke nyumbani aende shuleni, apewe kila kitu pencil, rubber kila kitu aketi asomezwe kila kitu.

**Com. Asiyo:** Pendekeza.

**James Kibwanga:** Napendekeza nini - Serikali ikisema ni bure iwe ni bure.

**Com. Lenaola:** Hadi kiwango gani?

**Com. Asiyo:** Mpaka class gani?

**James Kibwanga:** Kuanzia nursery mpaka university level. Maanake, kwa sababu nyinyi mna pesa. Kwa hivi sasa unakuta mtu akienda University, kuna loan facility pale ama sivyo? Basi hata kama ni loan facility itolewe kwa secondary kama Serikali haiwezi kutoa secondary education bure, kuwe na loan facility ya form one mpaka form four. Lakini kutoka pre-primary mpaka class eight iwe ni totally free.

**Com. Asiyo:** Haya endelea.

**James Kibwanga:** Na upande wa elimu pia nitaguzia kwa sasa kuna matatizo haya ya Waziri wa elimu na walimu wake. Mimi napendekeza sheria ikipitishwa kuwe kumefanywa utafiti wa kutosha kwamba pesa iko ya kulipa kama ni walimu mshahara. Iwe imefanya utafiti wa kutosha. Lakini ikiwa itapitizwa tu na huko pesa hakuna, itakuwa ni shida. Kwa hivyo mimi napendekeza sheria yeyote katika nchi, isipitishwe mpaka utafiti wa kutosha ufanywe kwamba hiyo sheria inawezekana kutengenezwa ndipo sheria hiyo ipitishwe. Kwa hivyo sheria sisipitishwe tu hivi hivi, ili kujiepusha na matatizo ya kuwa sheria ilipitishwa na watoto wanalipa fee, na walimu hawapewi mshahara yao na mambo kama hayo.

**Com. Lethome:** Sema jambo lako la mwisho.

**James Kibwanga:** Msinikatizie nyinyi mumeongea mkatosheka. Upanda wa Utalalii: Upande wa Utalalii kwa vile Majimbo tunayo sasa - ama kama mtayakataa, kwa vile utalalii uko mwingi Pwani hapa sioni kwa nini college ya utalalii iwekwe huko Nairobi. Utalalii uko mwingi hapa kuwaanzia Tsavo mpaka huku Utalii mtumpu. Kwa hivyo hiyo college iamizwe kuwanzia hivi sasa, iamizwe ilitwe huku.

Nikiongezea, kama upande wa huko Bungoma kuna mahindi mengi, kama kutauundwa college ya mahindi ijengwe huku Kitale huko. Ya miwa huku Mhoroni huko, ya Utalalii hapa Mombasa hapa Pwani hapa.

Upande wa Judiciary, upande wa ma-judge, Uhakimu: Kwa sasa tunaona hawa; watu wanachaguliwa na Rais. Kuundwe Tume ya kuwandika kazi hawa, maanake mimi ukinipa kazi wewe :chukua kazi hii", basi mimi nitakuwa ndio Bwana, ndio Bwana, maanake nikipinga utanipokonya kazi. Ndio vile inaendelea na Rais wetu sasa. Wale ma-judge wanaogopa kwa hivyo ni "ndio Bwana, ndio Bwana" wanaogopa kukusa mkate. Kwa hivyo kuundwe Tume ya kuwandika kama vile Public Service Commission, Teachers Service Commission, kuundwe Commission - ya Judicary pia.

**Com. Lenaola:** Kuna Judicial Service Commission .

**James Kibwanga:** Inawaandika?

**Com. Lenaola:** Hipo.

**James Kibwanga:** Hipo lakini inawaandika?

**Com. Lenaola:** Ndio.

**James Kibwanga:** Haiwaandiki!

**Com. Lenaola:** ….. Judicial Service Commission ichaguliwe na nani? Kwa sababu Tume iko, kuna Tume.

**James Kibwanga:** Tukubaliane ichaguliwe na Bunge. Upande wa Defence: Mambo ya usalama; unakuta; na nina ushaidi wa kutosha. Siku zinazokuja kama hii Katiba mpya, ikiwa ni Coast Province, Kilifi District kunaandikwa ma-polisi, tuone Mijikenda watupu hapo. Ikiwa ni upande wa Kwale tuone Wadingo na Waduruma huko wanaandikwa.

**Com. Asiyo:** Polisi watakuwa wemetoka kule juu au ni wa hapa nchini?

**James Kibwanga:** Hapa hapa maanake……………

**Com. Asiyo:** Kutakuwa na Polisi Force ya juu?

**James Kibwanga:** Ni hivi; hata iwe kwa mfano sisi tunaendelea kuzungumzi hatujui kama Majimbo itakubaliwa lakini vile nasema, katika Serikali kuwe kunatangazwa tarehe fulani ma-polisi watandikwa Kilifi, basi tukute Mijikenda huko, sio tukute kina Kiprotich huko. Maanake twashangaa tuna Bahari hapa, Kenya Navy ni kina Ogot watupu wako hapa na kina Oluoch na Bahari ni yetu. Kwa hivyo kama ni Navy tunataka kina Salim, kina Kibwanga, kina Charo huko kwa Navy huko. Ningependekeza mengi lakini naona wakati, pia wenzangu wanataka kuongea.

**Com. Asiyo:** Tafadhali nenda pale mbele ujiandikishe kwa register yetu, ndio hapo utakuwa umetambulisha kila kitu.

**Com. Lenaola:** Lakini una swali, rudi pale, swali moja tu ndogo. Maneno yako haya umesema, ukishapata Serikali ya Majimbo ikiwa kuna mtu si mkaaji wa Jimbo lile asikubaliwe kununua ardhi pale?

**James Kibwanga:** Akodishe.

**Com. Lenaola:** Haya; Lakini kwa sasa, kwa mfano, mimi Jimbo langu ni huko Baharini, Lake Victoria lakini hivi sasa nina ardhi hapa Mariakani, sasa tufanye nini? Linyakuliwe ninyang'anywe?

**James Kibwanga:** Unyang'anywe. Hii Katiba itakunyanganya - maanake tufana over-hauling vile Mechanic wanafanya.

**Com. Lenaola:** Nitalipwa, sitalipwa?

**James Kibwanga:** Unaweza kulipwa pia lakini Katiba itakupokonya ardhi hii.

**Com. Asiyo:** Okay, asante sana Bwana Kibwanga. Ningependa kuwajulishini wote mliohapa leo asubuhi, kwamba Mheshimiwa Mjumbe wetu amefika na tunamkaribisha sana na tunafurahi kwamba amepata nafasi hii kuja kwa kikao cha kusikiliza maoni ya watu wa hapa - karibu sana. Tutaendelea mbele kusikiliza Bwana Salim. Bwana Salim Juma kama amechelewa, Gabriel Sumbi fika haraka kijana, fika mbele haraka na uongee; kwanza unaanza na majina yako yote halafu endelea kutoa maoni yako.

**Gabriel Sumbi:** Kwa jina mimi naitwa Gabriel Sumbi. Kwa kweli Katiba iliyoko sasa hivi ina mwelekeo…………………………..

**Com. Asiyo:** Hebu sema kwa sauti ya juu.

**Com. Lenaola:** Toa sauti kijana.

**Gabriel Sumbi:** Kwa jina naitwa Gabriel Sumbi na mapendekezo yangu ni kama haya: Hasa mimi ningeguzia upande wa Administration - level ya Chief na Sub-chief - Kwa kweli Ma-chief wengi walioko na ma-sub-chief ni semi-illetrate, kwa sababu utakuta mtu hakwenda School of Administration………………….

**Com. Asiyo:** Toa pendekezo.

**Gabriel Sumbi:** Pendekezo langu ni kwamba Chief yeyote ama Sub-chief yeyote iwe ame attend School of Administration with at least a qualification of a certificate.

Pili, katika hizi Chief's camps na Sub-chief camps utakuta kuna wazee ambao ni illetrate wameletwa pale kuwamua kesi za wananchi. Na wale wazee hawakusomea sherai yeyote. Kwa hivyo, pendekezo langu ni kwamba wale wazee wasiruhusiwe kukaa kwa camps za Chief. Kwa sababu wana promote corruption.

**Com. Asiyo:** Unapendekeza aje?

**Gabriel Sumbi:** Pendekezo langu ni kwamba wasiwe katika camps za Chiefs.

**Com. Asiyo:** Nani atafanya hizo kazi ambazo wanafanya?

**Gabriel Sumbi:** Kwa sababu tutakuwa na Chief ambaye amefanya Administration, atajua jinsi ya ku-handle hizo kesi.

**Com. Asiyo:** Yeye mwenyewe?

**Gabriel Sumbi:** Yeye mwenyewe binafsi kwa sababu amesoma.

Pili, ningeguzia upande wa MPs – MP hata kama term ya Bunge ni miaka mitano, lakini unakuta kwamba MPs wakishapata zile kura wakingia kule Bunge, washasau wananchi

**Com. Lethome:** Pendekezo.

**Gabriel Sumbi:** Pendekezo langu ni kwamba, iwapo MP atasahau watu wake wananchi waweze ku-forward their grievances tu a Commission ambaye itateuliwa na Serikali, yule MP afukuzwe. Because amechaguliwa na wananchi.

**Com. Asiyo:** Haya tumeelewa

**Gabriel Sumbi:** Pili Judiciary: Judiciary hasa tunaona ina-favour wale matajiri. Kwa sababu mawakili ni pesa. Pendekezo langu ni kwamba, kuwe na a group of Advocates ambao hao watalipwa na Serikali kushugulikia masikini. Wale ambao hawawezi kufungua ma-file kwa mawakili na wale ambao hawawezi ku-chase their cases in court.

**Com. Asiyo:** …endelea

**Gabriel Sumbi:** Halafu tatu, hii mishahara ya Wabunge iko juu sana na kuna masikini wanakufa njaa mabarabarani.

**Com. Lethome:** Pendekezo?

**Gabriel Sumbi:** Pendekezo: Kuwe na Commission independent ambayo itapanga mishahara ya Wabunge. Asanteni.

**Com. Asiyo:** Asante sana; usiende bila kuwandika jina lako hapo mbele. Okay sasa tutamsikiliza, - kama Bwana Salim ameingia - kama hajaingia bado tutamsikiliza Bwana Stanley Mumo. Stanley Mumo atafutwa na Salim subah. Tutafika mpaka saa sabu unusu tutoke kidogo kwa nusu saa halafu turudi.

**Stanley Mumo:** Kwa majina naitwa Stanely Mumo. Pendekezo langu la kwanza ni kuhusu powers za Police, Naona Police wana powers nyingi sana wanaonea wananchi wa chini. Kwa hivyo powers za Police kama inawezekana zipunguzwe.

Ya pili ni Chiefs na Ma-councillors - Education yao iaanzie form four with at least minimum of D+.

**Com. Asiyo:** Ma-chiefs?

**Stanley Mumo:** Chiefs na ma-Councillors.

**Com. Asiyo:** Wawe form four?

**Stanley Mumo:** Form fours with a minimum of D+ kwa sababu hatuwezi kuongozwa na mtu ambaye, somebody who never stepped the inside of a class. Nomination of Mayor ifanywe na wananchi sio ma-councillors, because the mayor anaweza ku-corrupt Councillors wampigie.

Kitu kingine ni job security: In Kenya we have no job security, mtu anandikwa kazi na tajiri wake na aweza kukufuta hata ukiwa ndani ya basi, anakwambia, "kesho I don't want to see you" – na ukienda kwa Ministry of Labour, unapata wame-corrupt. He is ready apewe 20,000/= akunyime wewe 5,000/=.

Education sponsorship: kuna ma-bursary; zile bursary zinazotokea hasizaidii masikini. Kwa hivyo ikama kungeweza kuwa na Commission ambayo ita-monitor bursary zipewe wale masikini and not the rich. Because bursary inatoka ipewe wale masikini.

Halafu seperation of powers: Tunataka powers za President zipunguzwe maanake President wetu ana powers nyingi zaidi.

Nyingine fair recruitment: When it comes to recruitment of forces unakuta kuna watu wanaleta watu wao. We have been there, tunaona kuna MP analete watu wake wanne, kuna wakubwa fulani wanaleta wao katika recruitment, wanachukuliwa hao first. Kwa hivyo tunataka kuwe na fair recruitment kama kuna Commission itafanywa, iwe ina-monitor hizo recruitment. Halafu pia when it comes to Police, pia kuwe na Commission ambayo itachunguza; police anafanya uhalifu mahali, halafu kunatumwa polisi aende akachunguze, will it be fair? Police ambaye were ni same college amefanya kitu kibaya halafu mwenzeka anatumwa alete report mbaya. Tunataka independent body ambayo itakuwa iki-monitor movement za polisi.

**Com. Asiyo:** Endelea.

**Stanley Mumo:** Halafu nyingine ni MPs, kuhusu mishahara yao: Naona si haki MPs wakae wa-decide mishahara yao wenyewe. Nataka kuwe na Chama ambacho kitakuwa kinakaa kinaamua mishahara ya wanafanyi kazi wa Serikali wote. Asanteni.

**Com. Asiyo:** Okay. Asante sana pitia hapo uandike majina yako yote na uweke sahihi. Sasa Bwana Stanely amemaliza; nitamuita Salim Thuba na wewe Bwana Joseph Karinja ukae karibu.

**Salim Thuba:** Kwa jina naitwa Salim Kithuba nina mapendekezo yafuatayo. Kwanza ninapendekeza Serikali ya Majimbo katika kiwango cha Mkoa. Rais atakayechaguliwa awe na umri kati ya miaka thelathini na tano hadi sitini na tano. Rais na Mawaziri watakaopatikana na kashifa yoyote ya ufisadi, wawachizwe kazi mara moja na kupelekwa mahakamani.

Ardhi: Kila sehemu iwe na Kamati ya wazee ambao itakuwa ikisimamia mambo ya ardhi. Kila kijiji kiwe kitachagua Kamati ya maendeleo, ile tunaita “Village Development Committee”, na kamati hii iweze kutambuliwa na serikali na ndio itakayokuwa ikipokea pesa za miradi ya maendeleo

**Mheshimiwa Chibule Wa Tsuma:** Kwa jina naitwa Chibule Wa Tsuma. Kazi yangu ni utibabu na niliwahi kuwa Mbunge wa Kilifi South kwa vipindi viwili na hivi sasa niko uwanjani. Ninagombania U-rais kwa tikiti ya Federal Party of Kenya, na Ubunge kwa tikiti hiyo hiyo. Nitaanza.

Nchi za dunia zimegawanywa mara mbili ki-uchumi; kuna developed Countries and developing Countries. Zile developed Countries, wale wananchi pale wanapata masilahi yao ya kuendesha maisha yao - chakula cha kutoshana na afya zuri - kazi na kama hawana kazi wanapata chakula hata kama ni Serikali kulipa. Developing Countries ni kama hii yetu - bado tunang’ang’ana na basic maintenance of life. Mwaka wa sitini na tatu tulipata uhuru na mwaka huo wa sitini na tatu Kenya kimaendeleo, ilikuwa sawa sawa na Singapore, South Korea, Tai-wan. Sasa mwaka wa elfu mbili na mbili ni miaka arubaini imepita. Tuangalie kimaendeleo Kenya bado iko pale pale ilikokuwa - pengeni haiko pale; inaenda kinyume-nyume. Lakini Sengapore, Tai-wan na South Korea sasa zimeingia ile group ya developed Countries - Economic Tigers. Sasa, ni kitu gani kimepita hapo mpaka ikawa hivyo, na tulipokuwa tunachukuwa uhuru tamaa yetu ilikuwa ni maendeleo?

Sasa hapa pana zimwi, kuna zimwi tulilotia chupani wenyewe. Sasa zimwi halitaki kurudi chupani na zimwi lina njaa, linataka kutula sisi wenyewe, tutafanya aje? Zimwi maana yake ni ni nini? Ni ufisadi or corruption. Corruption ndio ambayo imetapakaa, ikaenea na ndio ambayo imeshika Kenya kwa koo mpaka Kenya inatapatapa. Na hiyo imezababiswa na nini? Kuna Bwana mmoja mtaalamu wa siasa, jina lake Lord Actom ambaye alisema; “Power corrupts and absolute power corrupts

absolutely"; maanake ni kwamba uwezo wa Serikali ule unaoendesha nchi ili nchi inufaishe wananchi, ni kama mvinyo, ni kama pombe, pia nayo hulevyesha; na ukiwa umepewa kindudu cha pombe ya mnai peke yako ung'ang'ane nacho, mwisho utalewa zaidi na utakuwa huwezi.

Sasa shida ilioko hapa, ni kwamba mipangilio yetu ya ule uwezo wa Serikali ambao unaendesha nchi ni wrong. Mipangilio yetu ni wrong - a lot of power has been given to one place or one person na wamelewa wote; ndio sababu tuko kwa taabu. Sasa mimi naona ya kwamba hapo ndio penye shida na sasa tunachora Katiba, Katiba ni mkataba, ama mapatano kati ya wananchi na Serikali, na kati ya wananchi kwa wananchi. Sasa tunataka kuandika Katiba ambayo inaweza kuondoa hili zimwi na kulirudisha kwa chupa tufunge chupa, tulitupe Baharini tuwe salaman. Na mimi naona njia ya pekee ni ile niliyoshikilia - lazima tujue kitu kimoja; Katiba haiandikwi tu kiholela hivi - Katiba si kama Budget; kila mwaka tunayo, kila mwaka tunayo - nchi nyingi za dunia zina Katiba moja tu. United States of America imekuwa taifa tangu seventeen seventy two iliandika Katiba hapo na haijambadilisha - inafanya small amendments. Na sisi je? Tulipokuwa tunakuwa Taifa tulichora Katiba ama hatukuchora Katiba? In 1963 ndio tulipata uhuru December 12. Tulikuwa tuna Katiba ama hatukuwa nayo? Tulikuwa tunayo - tulikuwa tumechora wenyewe.

**Com. Lenaola:** Tafadhali Daktari, I will interrupt you. Unajua tunakata kumaliza tafadhali utatuwia radhi.

**Com. Asiyo:** Utatusaidia sana ……………………..

**Mheshimiwa Chibule Waisuma:** Kwa ufupi napendekeza Majimbo - yaani Majimbo vile yanavyofanya, ni ule uwezo wa ki-Serikali unagawanywa. Sehemu hizo za Serikali ni kama tatu lakini kwa moja, kwa sababu zinatumikia mtu mmoja. Sehemu ya Central Government, sehemu ya Regional Government, sehemu ya Local Government - na hiyo tuli-propose wakati wa uhuru - hautuka-propose tuli-endorse hiyo Katiba. Lakini haikupewa nafasi - ili kurofishwa na ma-agents wa hili zimwi, wengine walitafuata hili zimwi wakalitoa, zimwi la ufisadi ndio waka-veto hiyo Katiba ya Majimbo. Kwa hivyo mimi recommendation yangu haswa, ni kwamba mambo mengi yanastahili kufikiriwa wakati wa kuandika Katiba. Lakini mimi ninaamni kuna moyo wa Katiba, kuna shina la Katiba, kuna umuhimu wa Katiba; ndio ule sasa tuna involve wananchi. Hayo mengine mengeni small small details, tuna mawakili na wazee kama Lenaola ambao wanaweza kutujazia jazia yale mahitaji. Lakini ule mti, sasa ile sisi tunataka ku-propose kama wananchi ni Majimbo - devolution of power. Hii mvinyo igawanyiwe watu ili wazilewe ili waendelee kututumikia vizuri.

Na nilikuwa na propose hivi; katika hiyo Majimbo Government kama vile ilivyokuwa proposed, ingekuwa hapa Mombasa tutakuwa na mtu kama PC lakini tutampa jina jingine, kwa sababu hatakuwa ni mtu tumemchagua kwa muda wa miaka mitano na yeye hatakuwa na uwezo direct kutoka kwetu - sio kuchukuwa instructions kutoka Nairobi. Kule America kuna Governors ambao wamechaguliwa na wananchi wa ile sehemu. America ni 51 Jimbos. Sisi wakati wa uhuru tulikuwa Majimbo manene, sasa pengine kwa sababu ni miaka arubani tangu uhuru tunaweza kufikiria kama tutayaongeza yakawa kumi, kumi na moja

namna hii, lakini ile spirit iwe hiyo hiyo. Na huko kwingine kama Ma-chief wanachaguliwa na wao pia na mambo mengine. Sasa kwa ufupi that is my point.

Iko hii nyingeni tunasikia huko watu wanapagina kuhusu President awe na more power than Prime Minister, ama Prime Minsiter awe na more powers than President. Na mimi nikingalia hivi, naona ya kwamba hiyo yote ni sauti ya kuwambatana na lile zimwi. Sisi tunataka kupunguza ile power kutoka kule. The President there will not be as powerful as Moi is, lakini sio kwamba ati power hitatoka kwa Moi, iende kwa mwingeni ndani ya chumba hilo hilo, hapana! We want real and effective devolution of power. Ingine itakuja Mombasa, ingeni itakwenda Nyanza, ingini itakwenda wapi na hata hapa Mombasa sehemu nyingine ya hiyo power itapelekwa Kilifi. That is what we want. Sasa mimi nafikiri, I better stop there. Thank you very much.

**Com. Asiyo:** Asante sana Mheshimiwa, kwa hayo maoni yako na weka sahihi yako hapo. Sasa tuko na Patrick Saburi; kuja utoe maoni yako na utoe mapendekezo.

**Patrick Saburi Wakamoti:** Kwa majina naitwa Patrick Saburi Wakamoti mimi ni Diwani kutoka Mugumo-wa-Pata Ward chini ya Mariakani Town Council. Tumekuwa na Kikao kibaraza, tumetengeza Memorandum ikiwa changizo yetu na nafikiri Councillor Hawad ameshazipeana, lakini kuna mengine ambayo hatuyaguza pale, na nimeonelea kidogo niweze kuyatoa.

Mapendekezo yangu kwanza ni Katiba tunayotaka kuwandika kwa sasa, iwe itakuwa ni ya Serikali ya mfumo wa Majimbo. Katika mfumo wa Majimbo tuwe na Central Government juu, chini tuna Regional Government halafu tuwe na Local Authorities chini yake. Kwa kusema hivyo ni kwamba, hawa Provincial Administration nguvu yao iwe haitamzidi elected representatives wa wananchi kama Councillor. Kwa mfano saa hii, ukiwa na mkutano wako kwa Sub-location au kwa Ward, na Assistant-chief hayuko radhi na ule mkutano anakuja kuuvunja na wewe umechaguliwa na wananchi - una mandate ya wananchi na yeye amefanya tu kuwa employment hapapo hata pengine hana support ya wananchi. Kwa hivyo ile nguvu ipunguzwe, elected person awe na nguvu kushinda yule. Kwa hivyo ndio tunasema Central Government, chini yake iwe ni Regional Government halafu Local Authorities - hawa Provincial Administration power zao ziwe chini ya elected representatives ya wananchi.

Nafikiri nitazungumza kwa ufupi maanake naona time zinakwenda na wezangu wengi wanataka kuongea. Nitarudi kwa umilikaji wa ardhi. Umilikaji wa ardhi uwe utaachiwa locals katika lile Jimbo. Na kuwachiwa locals ni kwamba, mambo ya squatters nafikiri tutakuwa tumeyapunguza ikiwa locals wenyewe watakuwa na nguvu ya kumiliki ardhi zao. Currently, saa hii local amekaa - pengine pale nimetoka amekaa tangu kuzaliwa kwake na baba yake na babu yake, na saa hii yeye hana Title-deed, na hapo jirani kuna wengine ambao wamekuja kununua juzi wanapewa Title-deeds mkononi na mwenyeji yuko pale miaka mia moja iliyopita, na hana Title-deed. Kwa hivyo jambo hilo ninafikiri kulipunguza ni kwamba hawa locals watambuliwe, wapimewe ardhi, mgeni akija kununua hiyo ni pesa yake amenunua hawezi kudhulumiwa. Lazima umilikaji apatiwe through legal procedures ambazo zitakuwa zimefuatwa.

Tukirudi upande wa elimu; pendekezo yangu ni kwamba elimu ya msingi iwe ya lazima na ya bure. Mtoto asionekane anauza tomatoes hapo Mariakani Township akiwa umri wa kwenda shule. Mzazi wake atafutwe na ashtakiwe kwa ajili mtoto hakwenda shule. Shule pia, Serikali isimamie kuwaanzia majengo na vifaa. Nafikiri kwa wenzetu hata hapa East Africa kuna Serikali zingeni ambazo kwa elimu ya msingi, Serikali inasimamia majengo, vitabu na vifaa vyote na malipo. Mzazi yake ni uniform na kuangalia afya ya mtoto wake. Kwa hivyo elimu iwe ya lazima na ya bure kwa Primary. Na ya Secondary, kuwe na viwango vya School fees maanake fees kwa sasa kiwango kinawashinda wazazi; kuna watoto wengi ni dropouts shauri ya kuwa wazazi wanashindwa na kumundu ile school fees. Kwa hivyo shule za upili, kuwe na kiwango cha nafuu cha malipo ya karo, ili watoto wote waweze kupata elimu ya Secondary.

Kwa upande wa afya, garama ya afya imekuja juu sana ndio maana kwa sasa unakuta wananchi wengi wanatezeka, mtu akishikwa na Malaria anakimbia dukani kununua tu Paracetamol na Asprins maanake ndio uwezo wake - anashidwa na kwenda hospitali ya Serikali kwa maana akifika pale, kwanza kuwandikwa card ni shilingi kumi, kupimwa damu shilingi arubaini, pengine mtu yule hata lunch yenyewe imemshinda nyumbani, inabidi yeye aende akanunue Paracetamol ya shilingi kumi aje ameze hali Malaria pengine haiwezi kuwa controlled na ile Paracetamol. Kwa hivyo ile cost sharing ya public hospitals iondelewe na afya iwe Serikali itasimamia kwa wananchi wote.

Kwa wafanyi kazi: Wafanyi kazi siku hizi matajiri wamekuwa na tabia ya kuwagadamiza wafanyikazi hasa kimshahara. Mfanya kazi yule atalipwa kiwango ambacho, yeye daily consumption yake haitosholeswi na ule mshahara. Kama tulivyosikia, kibarua wanalipa shilingi themanini na tano na kweli, na mtu anatoka mahali analipa tikiti ya shilingi ishirini kwenda na kurudi! Sasa, mfanyi-kazi hapo mbeleni alikuwa na bargaining power yake wakati akiona mambo yamezidi, mfanyi-kazi alikuwa ana-declare mgumo na mgomo ulikuwa unakubaliwa. Kuna wakati nilipokuwa nikifanya kazi mwka sabini na tatu hivi, tulikuja tukagoma kwa Kampuni, Tajiri akakaa na sisi na chama chetu cha wanafanyi kazi, mambo yakawa mazuri. Siku hizi mgomo umekuwa ni haramu, mfanyi-kazi akigoma anaondolewa, yeye kile anachopata hakimtosholezi: sasa yeye ataenda wapi kujitetea? Kwa hivyo nafikiri bargaining power ya mafanyi-kazi ingekuwepo, akawa na haki ile ya kukaa na tajiri wake na kuelewana.

Nitarudi kwa upande wa uchaguzi: Uchaguzi, maoni yangu ninapendekeza uchaguzi wa Madiwani, na Wenye viti na Ma-moyar uwe direct kwa wananchi. Na pia uchaguzi wa madiwani utenganizwe na wa Bunge. Madiwani wawe na siku yao ya kufanya uchaguzi wao, wananchi kufanya uchaguzi wa viongozi wao wa udiwani, na uchaguzi wa Wabunge na Rais uwe na siku yao. Katika uchaguzi ujao, mapendekezo yangu ni kwamba Rais akayechaguliwa asiwe above the law. Akifanya makosa sheria iwe na haki ya kumshtaki. Pili, mambo ya uteuzi wa viti kama Mawaziri, Mabalozi na viti vile vya Ki-serikali visimamiwe na Tume Maalum, isiwe ni Rais. Kuundwe Tume Maalum ya kuteua Mawaziri kulingana na ujuzi wa kazi - pengine ni Ministry of Health, tupate Daktari ambaye anaweza kusimama pale, akaongoza hiyo Ministry vizuri. Balozi hali kadhalika, tume iwe inaweza kuchagua ni nani ataweza kumpeleka mahali fulani kwa kazi fulani.

Upande wa ukulima; ardhi yetu sisi hasa hapa Pwani, nafikiri sehemu kubwa haina ma-title-deeds. Basi hivyo wakulima wanashindwa na kupata mikopo ya kujendeleza. Mapendekezo yangu ni kwamba kwa kuwa wengi hawana ma-title-deeds na wanataka kujiendelesha hasa ki-ukulima ndio waweza kutosholiza Kenya hii kwa chakula kuwe na udhamini kutoka kwa mabaraza, kuwadhamini wale wakulima wapate mikopo mahali ili waweze kujiendeleza. Yaani mkulima akitaka loan aweze kupitia kwa Local Authority ambayo itampatia kartasi ya udhamini aweze kupata loan ya kumendeleza ki-ukulima. Maanake, tukingojea Title-deeds tunakaa muda mrefu na Title-deeds hatuna, hivyo basi inabidi tubaki nyuma kila wakati.

Upande wa mishahara ya Wabunge na Madiwani; mimi pendekezo langu ni kwamba hawa wote, kuwe na Tume maalum ya kuchunguza hiyo mishahara wala sio wao kukaa na kujipendekeza kwamba walipwe kiasi fulani - lakini kuwe na Tume maalum ambayo itapendekeza mshahara wa Mbunge kulingana na kazi yake, mshahara wa Diwani kulingana na kazi anazofanya. Na malipo hayo pia ya Madiwani na Wabunge yatoke kwa Serikali, maanake wakati huu tunaambiwa mishahara ya Madiwani inatoka kwa mabaraza; kuna mabaraza mengini yana miezi sita hawajalipa madiwani wao. Kwa hivyo tunasema mishahara ya Madiwani na Wabunge itoke kwa Serikali, ili naye aweze kupanga maendeleo yake na wananchi wake kule. Maanake kuna misaada mingi ambayo Diwani hufuatwa na wanachi awasaidie - sasa kama yeye mwenyewe hajapokea atamsaidia nini mwananchi? Kwa hivyo itoke kule ili mwisho wa mwezi awe anaweza kupata na kupanga mipango yake. Kwa hayo machache asanteni.

**Com. Asiyo:** Asante sana Councillor Saburi. Kwa sasa tutamkubalisha Mheshimiwa Bwana Keah alikuwa amejiandikisha mapema sana.

**Mheshimiwa Keah:** Sijui nizungumuze Kiswahili, Kingereze - Kingereza ndio ingekuwa mbuo mbio zaidi.

**Com. Asiyo:** Ongea tu lugha yoyote ambayo unataka.

**Mheshimiwa Keah:** Sawa, hata Ki-giriama - maanake itaeleweka hapa. Asanteni Tume. Kwa ufupi kwa majina mimi ni Mheshimiwa Matheas Keah, Mbunge wa Kaloleni na Waziri mzaidizi wa Ministry ya Transport and Communications. Niko hapa na baadhi ya maoni ya wananchi wa Kaloleni - sio maoni yangu mwenyewe binafsi, lakini baadhi ya wananchi wa Kaloleni, tumekutana kule Kaloleni tukazungumuza, tukajandiliana mengi na nitatoa ……….
Wewe namna gani wewe, hauna heshima – all the time?

**Interjection from the audience**

**Com. Lenaola:** Excuse me ……………Can we respect the views of each other please.

**Hon Keah:** Wewe namna gani, wewe huna heshima all the time!

**Speaker:** Sisi watu wa Kaloleni tuko hapa……………………..

**Com. Lenaola:** Ngojeni, hiki kikao ni chetu sisi kama Tume ya Kurekebisha Katiba…………

**Speaker:** Sasa wananchi wa Kaloleni tuko hapa ……………

**Com. Lenaola:** Ngoja, ngoja, kikao hiki sisi ndio tunaendesha. Kikao hiki kimeitishwa na Tume ya Marekebisho ya Katiba, hakikuitizwa na Mbunge wala mwanasiasa yeyote. Kwa hivyo tafadhalini tuheshimiane, utapewa nafasi yako utatoa maoni yako……….

**Speaker:** ……………..(Inaudible)

**Com. Lenaola:** Kila mmoja atapata nafasi yake.

**Speaker:** Lakini atoe yake asitoe yetu…………………………….

**Com. Lenaola:** Sasa tuachie sisi, tuachie sisi Bwana, tafadhali. Asante endelea

**(Clapping)**

**Mheshimiwa Matheas Keah:** Tume ya Katiba mimi ni Mbunge wa Kaloleni, nimekutana na wananchi wa Kololeni, tumeketi na yafuatayo ni baadhi ya maoni yao. Ninayatoa hapa kwa ufupi sana, kesho mtayapata kimaandishi. Kesho tutawapatia tu memorandum. Lakini wacha hivi nipetie vichwa vile muhimu kwa dakika hizo tano au kumi mtakazo niachilia.

Ya kwanza, ni Preamble ya Constitution inaitajika. Preamble izungumze kuhusu Peace, Love and Unity - iunganishe viongu hivi kwa wananchi, iwe ndio vision yetu ya Kenya. Wananchi watawaliwe ki-democracia na pia vile vile kwa wananchi iwe ni Serikali of the people, by the people, for the people hiyo iweze kuingizwa katika hiyo Preamble. Preamble itambue tumetoka wapi kutoka independence mpaka wakati huu na pia Preamble ione jinzi ambavyo Harambee spirit imetekeleza hapa Kenya na ipatiwe mahala pake lakini kuwe na modifications katika spirit hiyo. Pia, ilihakikishwa kwamba kuna equitable economic development ya watu wote katika nchi ya Kenya.

Point ya pili tunasema hivi; Ya kwamba tunaitaji katika Katiba hii, National Philosophy yetu na guiding principles, nimesema tayari ni Government of the people, for the people, and by the people. Na pia tunataka human rights ziweze kuheshimiwa kwa kila Mkenya. Tunataka freedom of worship and association na worship hii ni worship ya mwenyezi Mungu, sio devil worship -

hiyo tumesisitiza kabisa. Na pia tunataka Sovereignty ya nchi yetu; pia vile vile, tunataka Rule of Law iwe kwamba inaheshimiwa na kila mtu.

Tatu, Constitutional Supremacy tunasema hivi; 65% ya Wabunge wote majority, ndio iweze kugeuza Katiba kama ilivyo hivi sasa. Tunaelewa ya kwamba kwa ajili ya vyama vingi, kuipata hiyo 65% ndio hiyo inatoa checks and balances. Lakini tunataka Katiba iseme hivi, hata jambo tunawapa Wabunge ruhusa hiyo, wasichezee chezee Katiba na kuibadilisha mara kwa mara. Na ikiwa kuna vifungo ambavyo tutavitoa kesho, ambavyo hivyo vikinguzwa, basi vifungu hizo ni lazima Katiba iende kwa wananchi - kuwe na Refenrandum - na hivyo tutawapatia kesho.

Citizenship: Automatic citizenship ya Mkenya, ni ile ambayo baba ni Mkenya na mama ni Mkenya - hiyo ni automatic bila kupingwa. Pia vile vile, Mkenya akiolewa na foreigner awe mke au mume, basi mtoto aliyezaliwa pale ana uhuru wa kuwa Mkenya au achague taifa lile apendelo - uhuru uko hapo. Lakini asinje akabaguliwa. Pia vile vile Mkenya akiolewa au akioa, yule mwenzake akipeana application, basi yule ikiwa ni mtu wa tabia nzuri anaweza kuruhusiwa. Application ile itapelekwa kwa Immigration department wachunguze uzuri wa Bwana yule au Bibi yule na manufaa yake kwa Kenya.

Nyingine tunaingia katika Defence and National Security; tunasema hivi sisi:- Recruitment katika Defence Forces ziwe kwa quota system. Kila Jimbo lipewe idadi sawa ya watu ambao wata-serve katika Defence na katika National Security. Hata Polisi, Army, Navy hayo yote. Lakini tulipo ingia Navy, tukasema ya kwamba Navy iko hapa Baharini, iko hapa Pwani na watu wa kutoka hapa Pwani, Navy wazidi zaidi. Lakini kwa vile ni National Defence Force basi hiyo tusema ya kwamba - watu wa hapa wa Kaloleni wamesema, tunataka wengi wawe watu wa Kaloleni. National Youth Service iendelee lakini hata hiyo pia iwe in quotas.

Halafu tukitoka hapo, tunaingia President aendelee kuwa Commander-in-chief wa Armed Forces. Lazima kuwe na mtu mmoja ambaye anaweza kumbofya ile kipengeleo ili asema sasa Kenya ina vita na nchi nyingine au sasa hakuna vita. Lakini kuwe na Defence Council ambayo itamshauri; Na powers za emergency pia vile vile, Rais awe na uwezo huo, lakini awe na Advisory Council ambayo itakuwa ni watu maalum watakaochaguliwa wenye ujunzi wa mambo hayo.

Political parites ndio nyingine: Political parties ni lazima shuguli yao iwe ni Political mobilization. Hata hivyo Katiba iseme ya kwamba, formulation na management ya political parties zifanywe na parties zenyewe, lakini watilie mkazo Social, Economic development zaidi ya hiyo siasa ya Political mobilization. Pia kuwe na discipline katika kila party. Yaani Katiba iseme kila party i-discipline watu wake na iwe imperative kwamba kila party itakuwa sio watu leo wahame kutoka KANU, kesho aingie FORD, kesho kutwa ni DP - umalaya ule sisi twasema Katiba ikomeshe. Kusiwe na limitation ya Political parties. Finance ya Political parties, wajaribu wenyewe Harambee zao waweze kwenda kutafuta huko wanakoweza kutafuta lakini wapate hizo Harambeee zao. Yaani financing isitoke katika mfuko wa Serikali.

Structures na systems za Serikali, twasema hivi sisi: Tunataka Serikali ya Majimbo iweko. We want a Federal system of Government - yaani Majimbo, na Majimbo haya participation kuwe na governance ya watu wenyewe - locals wawe pale. Na kuwe na checks and balances kati ya Serikali ya Majimbo na pia vile vile Serikali kuu. Kuwe na accountability, responsibility na good governance, hayo yote yatajwe katika Katiba hiyo ambayo tunaiandika hivi sasa. Rasilmali ambazo ziko katika Jimbo zitumiwe kwanza katika kunufaisha Jimbo hilo halafu sehemu yake iende kwa Serikali kuu. Kwa mfano hapa Pwani, Badari - mapato ya Badari sisi hapa Pwani hatuna kahawa, kwa hivyo kahawa yetu ni Badari, ndiyo tuliyopewa na Mwenyezi Mungu. Mapato ya Badari yawe kwanza sehemu kubwa, hata wanasema watu wa kaloleni 90% of the revenues ziwe hapa na 10% ndio ipelekwe huko Central Government. Katika kazi ya Central Government itakuwako vitu kama Finance, National Defence, Elimu ya Universities mambo kama yale - na hapo tuko open kujandiliana vitu gani zaidi Central Government ipeanwe. Okay, lakini kuwe na definite responsibilities kati ya Serikali ya majimbo na Serikali kuu kule.

Tumesema Land and Natural resources ziwe ni mali ya Jimbo. Pia tumetaja kuhusu mambo ya land adjudication kama ardhi. Ardhi ipeanwe kwa wenyeji pale, lakini wenyeji ambao wako hapo kwa wakati huo wanazo Title deeds - sio wale absentee Landlords. Hiyo ikomeshwe - hakuna jina la squatters litakalokuweko katika vocabulary ya Kenya tena.

Squatter! Hakuna kitu kama squatter. Kuwe na transition ambayo itahahikisha ya kwamba watu walio na ardhi hapa wanaitumia kwa manufaa ya hapa. Sio uwe na Title-deed ya hapa Pwani, halafu uchukue mkopo uende ukatajirishe kwingineko - tajirisha papa hapa kwanza. Ma DDC Chairmen na Heads of Department wawe watu wa hapa.

Tukiendelea tunasema ya kwamba, Katiba i-protect pia minorities na watu ambao ni marginalized groups. Wale watu ambao wako disabled itambue kabisa na iwapatie manufaa jinsi inavyowezekana.

Tunataka independent Conmmittee ambayo itatazama mambo ya mishahara ya Wabunge, sio Wabunge wenyewe wajikatie mishahara yao.

**(Clapping)**

Katiba hii, inasema hivi, kule bungeni kina mama wapewe angalao kina mama watano kutoka katika kila Jimbo automatic waingie kule. Kwa hivyo tukiwa na Majimbo manane, hao ni kina mama arubaini. Na kina mama wenyewe kutakuwa na rules na modalities ya vile watakavyochaguana katika Jimbo kina mama hawa watano. Na pia disabled waweze kupatiwa nafasi kule zisizopungua moja moja katika kila Jimbo; Kuwe na angalao disabled mmoja. Na pia youth mmoja mmoja kutoka katika kila Jimbo………………………

**(Interference from a person among the Audience)**

**Com. Lenaola:** Tafadhalini mkutano mmoja tafadhalini…………………………

**Com. Asiyo:** ………………..nobody interfered with you when you were talking; when you were talking nobody interfered with you. Please just respect whoever is talking. Nobody interefered with you. That's a very bad record that you are setting at this place. Ulipokuwa unaongea watu walinyamaza kabisa, sasa wewe umemaliza yako wacha mwenzako pia aongee - hiyo sio desturi nzuri.

**Com. Lenaola:** Tunarekodi kila kitu hapa. We are going with a very bad record of …

**Speaker:** Mr. Chairman nakuuliza swali anasema tulisema, tulisema wapi?

**Com. Asiyo:** Hapana, alikuwa na watu wake akiongea.

**Speaker:** Watu wake ni sisi………..

**Com. Asiyo:** No, no anao watu wake …………….

**Audience: (Clapping)**

**Com. Asiyo:** Sikiliza, kuna yule jamaa ambaye aliongea kwa niamba ya Waisilamu, sio kwamba kila Muislam alikaa pale akasema aje aongee mambo yake - huyu pia ni Mbunge wa hapa ana watu wake – mpe nafasi aongee.

**Com. Lenaola:** Endelea Mheshimiwa.

**Com. Asiyo:** Peana Heshima.

**Mheshimiwa Matheas Keah:** For the records, nilichaguliwa ma watu elfu ishirini - huyu hakuwa mmoja ya wale watu elfu ishirini. Kwa hivyo anipe nafasi ni nizungumze kwa niamba ya wale watu elfu ishirini walionipigia kura - huyu hakuwa mmoja wao. Thank you.

Okay; tunaingia katika Legislature; tunasema hivi; Parliament i-vet Constitutional offices na Ma-commissioners na Ministers wakati wa kuchaguliwa ninamini ya kwamba tutakuwa na Serikali ambayo itakuwa na President na Prime Minister. Prime Minister au President watachagua ma-ministers. Hivi sasa ni mtu mmoja anachagua ambaye ni Rais. Kwa hivyo; Prime Minister au President, atachagua wale Ministers na Parliament ita-vet. Vivyo hivyo ma-Managing Directors, Permanent Secretaries na zile office kuu kuu hata Ma-judge pia vile vile.

Occupation ya MP - MP asiwe part-time na kazi yake haswa ni kutunga sheria Bungeni na kuwakilisha watu wake katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo. Entry age ya President tumesema ya kwamba iwe miaka arubaini na akishafikia umri wa miaka sabini na tano, asiendeleee tena. Education ya Mbunge iwe at least form four na President akiwa na Bachelors' degree or equivalent hapo itakuwa inatosheleza. Kuwe na moral and ethical qualifications - ni lazima ziweko. Mtu akiwa amekuwa corrupt na ameiba, mtu huyo hafai kabisa kuongoza nchi hii. Na pia vile vile mawaziri wakishikwa na hatia za corruption na mambo kama yale, watolewe pending court action. Pia vile vile, tumesema President awe na uwezo wa ku-dissolve Parliament - awe na uwezo huo; lazima tuwe na nyanja hizo. Halafu Wabunge na President wa-declare assests zao, waseme utajiri huo wameupata namna gani.

Halafu tukienda katika the Executive, Constitution iweze ku-specifiy qualification hiyo. Tushasema ya President, na Vice President au Prime Minister na hata pia vile vile Mawaziri - hiyo nitaipitia number seven.
Wacha nisongee mbele; Judiciary, present structure iko adequate; tunasema hivyo kwa hivyo hiyo inaweza kuwa replicated into the present isipokuwa uteuzi wa ma-judge ni kwamba Rais anaweza kuteua, Prime Minister anaweza kuteua lakini Parliament iithinishe conduct ya watu wale. Tunasema Parliament kwa sababu Parliament ina representation ya Wakenya wote.

Local Government: Mayors wote waweze kuchaguliwa na wananchi sio Councillors. Nyingine nafikiri nitawapatia kesho ndani ya kimandishi, kwa hivyo nataka nichukue nafasi hii nisema asante - ziko nyanja nyingine ambazo zimebaki ambazo sijawapa……………………….. Human rights: Tumesema Human Rights kila mmoja apate Human Rights Kisawa sawa, ardhi mimezungumza vya kutosha, Culture - hiyo lazima niiseme iheshimiwe. Culture tunasema ni nini?

**Audience:** Utamaduni.

**Mheshimiwa Matheas Keah:** Utamaduni lazima uheshimiwe. Kenya ana diversity ya utamaduni. Katiba hii iheshimu utamaduni wa watu mbali mbali. Kama watu wa Pwani wana cultures zao ziweze kuheshimiwa, zesije zikazumbuliwa na watu wengine. Basi, nyingine nitazitoa kesho, nataka tu niseme hivi ya kwamba Ma-commissioners tunawasukuru lakini Tume, ni kwamba Civic Education haikuwa hali ile tulioitazamia iwe. Na wananchi wengi wamelalamika sana, kwamba ile Civic Education baadhi ya walimu hawakujua kazi yao ilikuwa ni nini, wengine walikuwa wanatoa tu advocacy badala ya kutoa ushauri wa Katiba jinsi itakavyo geuzwa hapa hivi leo. Kwa hayo machache nasema asanteni sana na Mungu awabarikie nyinyi wote.

**Com. Asiyo:** Asante sana kuna maswali hapa

**Com. Lenaola:** Swali la kwanza kuhusu the powers of recall kwa sitting MP - kwa sababu wananchi wengi wametoa maoni kama hayo. Tunataka kusikia maoni yako kuhusu jambo hilo

**Mheshimiwa Matheas Keah:** Limo hapa; Sikulisoma kwa sababu limo hapa katika memorandum hii mtakayoipata kesho. Wamechaguliwa kwa miaka mitano - wabaki hivyo hivyo kwa muda huo wa miaka mitano. Ikishamalizika miaka mitano, wananchi wanajua jinsi ya kumfanya Mbunge yule katili au Mbunge yule ambaye hakutekeleza wajibu wake.

**Com. Lenaola:** Haya hilo nilakwanza la pili kuhusu kumbuniwa ofisi katika kila sehemu ya wakilishi Mbungune, hile Mbunge awe na ofisi katika Constitutency yake na ofisi nyingine Nairobi. Je maoni yako ni aje?

**Mheshimiwa Matheas Keah:** Hilo pia lipo, sikuweza kulisoma na nakushuru. Tumesema hivi; kila Mbunge apewe ofisi na angalao mtu mmoja katika Constituency yake ili wananchi waweze kuwa na mahala ambapo wanaweza kwenda kupeleka maoni yao, vilio vyao na chochote kile ambacho wanacho. Na tena isitoshe, hata kule Nairobi pia, wawe na staff, maanake yako mengi yanayozungumzwa ya ki-utaalam ambayo Wabunge wengi yanawapita

**Com. Lenaola:**……..unapendekeza nini kuhusu swala hilo?

**Mheshimiwa Matheas Keah:** Tumesema hivi kwanza, Polisi wa Jimbo wawe wanatoka kwa Jimbo. Unyanyasaji wa Polisi pia hilo liko hapa - sikulisoma lakini wanasema hivi. Polisi anayenyanyasa wananchi afutwe kazi na kuwe na mtu mwingine kabisa, asiye Polisi afanye hiyo investigation. Maanake Polisi ku-investigate Polisi mwenzake itakuwa si sawa. Pia nataka niseme hivi, hasa hapa Kaloleni, ikome mara moja Polisi kunyanyasa wale wanaouuza Tembo ya Mnazi - hilo walisema wazi wazi. Wawache kunyanyasa watu wanaouuza mazao ya mti wa mnazi - moja ya mazao yale ikiwa ni pombe. Wacha kuwe na sheria za ku-guide lakini sio kuchukuwa mama anayetafuta School fees, halafu wamnyanyase. Hilo tunataka Katiba - ndio pale tusema Katiba ilinde rasilmali za kila Jimbo. Hapo ndipo ilipomaanishwa na ndipo ilipoingiliana.

**Com. Asiyo:** Asante Mheshimiwa.

**Mheshimiwa Matheas Keah:** Thank you very much.

**Com. Asiyo:** Sasa tuko na Bwana Kadenge. Bwana Kadenge ako? Atafuatwa na Kajuli. Ama Kajuli aliongea? Huyo aliongea? Halafu niko na Bwana Stanely Mwango. Nani Mwango? Kuja hapa mbele. Utafuatwa na P. L. Mzalai, halafu Catherine Mwathe; Utakuja nyuma ya Mzalai. Haya endelea Bwana Stanley.

**Stanley Mwangu:** Asanteni sana kwa kunipatia nafasi hii ambayo naona sana kuwa ni muhimu kwa sababu.

**Com. Asiyo:** Jina lako tafadhali.

**Stanley Kalu Mwango:** Kwa majina naitwa Stanley Kalu Mwango.

**Com. Asiyo:** Endelea sasa Bwana Stanely.

**Stanley Kalu Mwango:** Nashukuru sana kwa nafasi hii, na naona mengi sana yamezungumzwa lakini nitaongezea kwa sababu mimi pia nilikuwa nimeandikisha.

**Com. Asiyo:** Eleza.

**Stanley Kalu Mwango:** Sehemu moja ambayo nilikuwa nataka kuongezea katika yote yaliozungumzwa ni kuhusu muundo wa Serikali. Muundo wa Serikali ambayo ninaona ni muhimu na nina sababu kamili, ni Serikali ya kimajimbo. Nasema Serikali ya kimajimbo - wengi ukisema Serikali ya kimajimbo wanafikiri wewe unataka ukabila - Hasha. Kitu ambacho nataka kuweka pale iwe wazi ni kwamba, Wakenya wenyewe - utaujua mti kwa matunda yake. Hata kama unaujua ni mti fulani, lakini ungojee kwanza, ukishatoa matunda yake utajua huu mti ni korosho ama ni mnazi.

**Com. Asiyo:** Pendekeza.

**Stanley Kalu Mwango:** Mwanzo nimependekeza Serikali ya majimbo lakini sasa natoa maelezo kidogo. Mwaka ule wa tisini na mbili wakati siasa ya vyama vingi ilivyokuja, niliona kwamba watu waliungana nyuma ya FORD na wengi sana walikuwa na hiyo "wave - wanafuatana nyuma watengeneze Serikali ya umoja. Lakini sasa walipoona kifungu kile cha 2A kimetolewa na hiyo Multi-party imeingia, kulikuwa na mikutano na katika hiyo mikutano ulikuta kwamba kila mtu alichukuwa "nyama" yake -alikata nyama yake akarudi kwao; yule akakata nyama yake akaenda Nyanza, yule akata yake…….

**Com. Asiyo:** Kijana unajua hiyo ni hadithi na watu wanaondoka. Eleza mapendekezo yako tafadhili.

**Stanley Kalu Mwango:** Kwa hivyo napendekeza kwamba Serikali hii ya Majimbo italeta uongozi karibu na hao watu katika Jimbo lao.
Halafu sehemu nyingine inahusu Presidency. Huyu kiongozi wa nchi, -itakuwa kwamba kila Jimbo litakuwa na Kiongozi wake ambaye ni Governor. Halafu kuwe na yule ambaye atachaguliwa ambaye hayuko affiliated kabisa na Jimbo lolote. Huyu pengine atawekwa katika arena ajizungumzie, ata-serve watu namna gani. Watu wamsikize kama kule America. Na watu wakimchagua basi yeye ata represent na yeye katika rassilmali za Majimbo ile sehemu itakayotokea kama ni 10%, katika Jimbo itaingia katika ile ofisi yake afanyie kazi katika kuwakilisha nchi yote sasa.

Jambo lingine ni kuhusu mambo ya ardhi, hili jambo wengi wamelizungumzia na ninataka tu kuongezea pia kwa sababu wengi wametoa mawanzo kama yale ambayo nataka kutoa. Ni kwamba, wengi wamezaliwa - hakuna anayechagua azaliwe wapi, ama akute hata pengeni ardhi iko namna gani, lakini anashukuru kwa sababu amezaliwe pale. Lakini sasa jambo la kushikitisha - hata wengine wanasema kuwa na ardhi ati ulizaliwa pale si kitu - huu ni upuzi mtupu. Lakini anakuja mtu mgeni anakuja akiwa

na karatasi, ama atakuja baadaye, aje alete machine pale achimbue chimbue - kuna vizingiti vimewekwa pale; anaambiwa huyo ndio mwenyewe na aliyekaa huko virago aondeke.

**Com. Lenaola:** Haya toa basi maoni.

**Stanley Kalu Mwango:** Kwa hivyo maoni ni kwamba, yule mwenyewe - wale wazaliwa waliozaliwa pale kwa sheria, maanake hiyo inasemekana sio written law - lakini ile ifanywe iwe written kama ni hivyo. Yaani ukizaliwa utambuliwe mahali ulipozaliwa na ardhi ile mwenyewe awe yule aliyezaliwa pale. Atatambuliwa yule hata kama ni kuuza auuze mwenyewe na kama ni Title-deed ile, yule atakayenunua ashiriki au mmoja wa mshiriki wa pale mahali sio kama mwenyewe.

Halafu sehemu nyingine ambayo nataka kuguzia ambayo ni ya mwisho sababu ziko nyingi sana, ni kuwa Serikali imeana ruhusa wengi wanzishe kazi kwa sababu ya ukosefu wa kazi – kuanzisha tuseme kazi fulani. Lakini sasa unakuta labda mama ameanza kazi yake ka kuuza tomatoe na ndio riski yake na Local Authority inawatosha ushuru na hawa tayari kazi wametafuta. Wach wakati tuseme peke yake lakini hizi charges zingine ziondolewe. Hayo ndiyo mapendekezo yangu.

**Com. Asiyo:** Asante sana hebu nenda pale mbele uweke jina lako kwa karatasi ile Kassim Mwalo.

**Kassim Mwalo:** Katika maoni yangu mimi kuhusu Marakebisho ya Katiba ni kwamba walemavu waweze kupewa umuhimu kwa sababu walemavu wamesauliwa sana. Na hata wakati yeye mamekwenda kwa elimu kwa chuo kikuu kwa mfano kusoma, akimaliza utamkuta anarandaranda hana mahali popote anaweza kupata usaidizi wa kuweze kujiendeleza mbele.

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo unapendekeza namna gani?

**Kassim Mwalo**: Ningependekeza walemavu wapewe umuhimu, hata nyathifa kubwa kule kama za kusimamia katika Ubunge, kama ni uongozi wapewe umuhimu sana.

**Com. Asiyo:** Ingine ni gani?

**Kassim Mwalo**: Kwa hivyo ikiwa watakuwa wamepewa umuhimu zaidi ndio tutakuwa tunajua nini katika matatizo ya walemavu wale wengine ambao watakuwa, wamesauliwa kule manyumbani, ambao wamefijwa mpaka dakika hii. Kwa hivyo ikiwa ni wakati kutakuwa na kiongozi wa walemavu, ni lazima wale watakuwa? Wamepatinakana kwa urahisi.

**Com. Asiyo:** Je ungependeza njia gani ambayo hawa walemavu wamefinywa wangeweza ………………..(inaudible) kuletwa ili wawe washiriki wa maendeleo ya nchi.

**Kassim Mwalo:** Katika maoni yangu wangekuzanywa mahali pamoja wale ambao wamezuiliwa manyumbani ili hata wapelekwe mashule ili waweze kupata manufaa yao. Maana kuna wengine hata dakika hii hawajafika shule - hawajulikani wako wapi na wako ndani huko.

**Com. Lethome:** Unafikiria kuna mashule ya kutosha ya kuwahudumia walemavu?

**Kassim Mwalo:** Shule ziko, lakini kuna wengine katika mwongozo sio rahisi sana kupatikana waende katika mashule; Pengine wale ambao watakuwa wana watu wao ambao wamesoma, wanajua maana ya ulemavu ni nini. Maana kwa ulemavu sio pengine kwamba ni mtu ambaye hatajiweza atakwa anajiweza na inatakikana walemavu wawe kama wale watu wengine wa kisawa sawa. Lakini kulingana na mwongozo ambao hauko, watabak pale pale.

**Com. Lethome:** Ukiangalia elimu ya wananchi wote kwa jumla kuhusu walemavu, unaona inatosha ama watu wote wa Kenya wanafaa kuelimishwa zaidi kuhusu mahitaji ya walemavu?

**Kassim Mwalo:** Inatakikana hao Wakenya wote waelimishwi ili hata wale walemavu watajua namna za kuelimisha wale. Ikiwa watakuwa hawakusoma, basi hao wengeni pia vile vile watabaki hivyo hivyo.

**Com. Asiyo:** …………………..(inaudible) kuna wengine ambao pengine wamekuja ………..(inaudible) je ungepeana mawaidha gani ili hawa ambao hawawezi kutembea waweze kupata ………….(inaudible).

**Kassim Mwalo:** Hawa wangepewa umuhimu wa kuweza kupatiwa hivyo vifaa naomba

**Com. Leneola:** Manyumba yetu kwa mfano ma-office, ma-hosipitali na majengo mengine ya umma ; je unaona kama yamejengwa kwa kufikiria hali ya watu kama hao wenye kutumia wheelchair na nini? Kwa mfano saa hii tukiwaambia uje hapa hivi na huna wheelchair unaweza kupanda hapa?

**Kassim Mwalo:** Siwezi.

**Com. Leneola:** Sasa manyumba yetu ya Kenya yanapojengwa, Luwa walemavu wanatikiriwa?

**Kassim Mwalo:** Hawafikiriwi.

**Com. Leneola:** Ungependekeza kitu gani?

**Kassim Mwalo:** Ningependekeza itengenezwe ili kuwa walemavu waweze kurahisishwiwa mahali ambako wanaweza kuingia. Hata kwenye vile vile ni shida kupanda kwenye magari.

**Com. Asiyo:** Umemaliza Bwana Mwalo?

**Kassim Mwalo:** Nafikiri hapo nimefika kikomo.

**Com. Asiyo:** Kuna mtu mwingine anataka kutoa maoni yake?

**Speaker:** Nataka niongeze kitu kidogo ambacho sikusikia mtu akiguzi.a

**Com. Asiyo:** Haya tafadhali nende kaa pale.

**Otondosson James:** Jina ni Otondosson James, kuna kitu ambacho pia ningependa kuguzia kuhusu philosophy. Philosophy tunayotumia hapa Kenya, ni philosophy ya "Harambee Nyayo", lakini ningependekeza philosophy ambayo Katiba inakuja iweke philosophia ya wananchi. Kama ni "wananchi juu", ni wananchi maanake hao wananchi ndio fundamental katika basic rights. Wananchi wawe represented namna hiyo itakuwa sawa.

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo philosophy of Kenya should be that of the people?

**Otondossor James:** Of the people yaani wananchi tu peke yake tu ndio nilikuwa naguzia.

**Com. Asiyo:** Unataka kuongea? ………….onegea basi, jina lako ni nani?

**Com. Lenaola:** Umeandikisha jina gani?

**Speaker:** Nimeandika E. M. Ebrahim.

**Com. Asiyo**: Kuja ukae nimekwita sana ulikuwa usikii

**Speaker:** Nilikuwa mbali.

**Com. Asiyo:** Haya endelea Bwana, unaweza kuongea lugha yeyote

**Ebrahim Mutahi:** Mimi ningetaka kuongea juu ya Majimbo. Hali ya Majimbo nikiangalia naona si nzuri kwangu au kwa wananchi wa Kenya

**Com. Asiyo:** Endelea endelea tu.

**Ebrahim Mutahi:** Kwa maana ukitoka mahali panaitwa Kisumu au Kitale kuja huku unalipa ukilipa mpaka ukifika Mombasa hauna kitu chochote utarudi na nini?

**Com. Asiyo:** Unalipa nini?

**Ebrahim Mutahi:** Ushuru.

**Com. Asiyo:** Okay. Kwa hivyo unasema kusiwe na taxation - kusiwe ushuru mtu akitoka Kitale mpaka Mombasa?

**Ebrahim Mutahi:** Mimi nasema ukitoka Kitale uje mpaka hapa, haya malipo yaondolewe kabisa. Ile ingine nitaongea kidogo ni ya shule – masomo. Masomo yale yako wakati huu si masomo, kwa maana masomo yaliyokuwa hapo mbeleni ya kutoka 1985 - hii 8.4.4……… Sasa nikiangalia naona mtu ako na degree pale, ananikuta pale ananiuuliza swali, gari hii yako unapiga moto nanma gani?

**Com. Asiyo:** Sasa unasema ……..pendekezo juu ya 8.4.4?

**Com. Lethome:** Itolewe?

**Ebrahim Mutahi:** Hiyo iondolewe irudishwe ile iliyokuwako zamani, hiyo ndiyo masomo. Na hayo masomo ya wakati huu, hata wewe ukingalia kwa TV wakati degree zinapeanwa pale, hakuna Mzungu pale hata mmoja, ni Mwafrika tu hapo. Yule mtoto wako na wangu tunapeleka pale washinde hapo, kwa maana hatuna mahali ya kuweza kuwapeleka, na hatuna pesa ya kuwapeleka Ng'ambo; Lakini ma MP na President, watoto wao wako huko wanasoma masomo yale ya kawaida.

**Com. Asiyo:** Sasa ungependekeza nanma gani?

**Ebrahim Mutahi:** Ningependa huo mfumo wa masomo uondolewe kabisa.

**Com. Asiyo:** Haya kitu kingine?

**Ebrahim Mutahi:** Kingine ni kiwa President asiwe above the law. Hiyo iondolewe.

**Com. Lethome:** Endelea.

**Com. Asiyo:** Ingine?

**Ebrahim Mutahi:** Sina lingine la kusema.

**Com. Asiyo:** Asante sana mzee kwa sababu ya yale umetwambia hebu kuja mbele uweke sahihi kwa mambo yale ambayo umetweleza na kwa wakati huu, Mabibi na Mabwana ningependa kuwapa asante sana, sana kwa kufika kwa kikao hiki ya Kamati ya Kurekebisha Katiba na kutoa maoni yenu ambayo tumeyachukuwa yote bila kukosea hata kimoja na ambayo tutaweka pamoja na mafikira ya watu wengine wa Kenya. Twashukuru sana na tunataka mtu mmoja atuombee kabla hatujatoka kwa mkao huu.

**Speaker:** Tungeomba kwa hisani yenu, kwa maana jinsi tumekaa na nyinyi na amani, tungejua viongozi ambao wamewakilisha (inaudible).Kwa maana naona iko Cassestte, kuna fulani fulani, pia tungependa wananchi tujue viongozi wetu ni akina. Tumekaa nao na amani namna hiyo.

**Com. Asiyo:** Wewe ulikuja umechelewa lakini tulieleza sisi nikina nani tulipoingia. Huyu ni Commissioner Lethome, Commissioner Lenaola, ambaye yuko kwa Kamati ya Katiba na pia Commissioner Lethome ambaye pia yuko kwa Commission hii ya kurekebisha Katiba na mimi – unasema unanijua – ni Mama Asiyo. Asante sana.

**Com. Lethome:** Na District Coordinator unamjua?

**Speaker:** Hapana.

**Com. Asiyo:** Huyo ndiye anawazaidia hapa

**Com. Lethome:** Daniel Mwaringa; na hawa ni Scretariat staff wetu wako hapa.

**Com. Asiyo:** Wanatuzaidia kuwandika mambo yote.

**Com. Lethome:** Tuko na Mrs. Patricia Mwangi yuko hapo, Racheal kazi yao ni kurekodi -hatutaki chochote kipite tuna Aminga, ni Program Officer wetu, we have a lady - Sign Language Interpreter kwa wale watu wako viziwi

**Speaker:** Na huyu ana-translate kama kuna mtu anaongea Ki-girima.

**Com. Lethome:** Kulipatikana mtu wa Ki-girima?

**Com. Asiyo:** Hakuna.

**Com. Lenaola:** Wagirima wote ni waswahili.

**Speaker:** Haya nimeshukuru asante.

**Com. Asiyo:** Sasa ni nani atatoa maombi ya mwisho kabala hatujamaliza mazungumzo ya leo. Maombi, maombi. Mtu mmoja ajitolee kutoa maombi ili tubarikiwi tukienda pande zetu kule tulikotoka. Kama hakuna basi Bwana Lethome tuombee.

**Com. Lethome:** Haya basi hebu tuombeni. Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwenye kuomba Bingu na Ardhi, tunakushuru wewe Mwenyezi Mungu kwa kikao hiki cha leo na tunakuomba yale yote yamezungumzwa hapa, yawe ni yenye manufaa kwa nchi hii. Tanakuomba uzidi kuibariki kazi hii, ni kazi muhimu sana na tunaomba umwepushe shetani na kazi hii na mitihani mingi ambayo anakabithi kazi hii. Mwenyezi Mungu tunaomba utuepushe nayo. Kazi yenyewe ni ngumu lakini tunajua tukiwa na wewe Mwenyezi Mungu na baraka zako, tutaweza kufaulu. Kwani ulisema yeyote atayekutegemea atafaulu bila shaka. Tunakuomba kila mmoja wetu atakapoondoka hapa, umfikishe mahali anapokwenda kwa salama na sisi pia tunakuomba utubarikie na uweze kutufikisha sehemu nyingine kwa amani na usalama, na utuwezeshe kuwandika Katiba mpya kwa sababu ya vizazi vijavyo. Tunaomba hayo yote tukiamini Mwenyezi Mungu kuwa utatusikia, Amina.

Meeting ended at 6.00 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**